Ijumaa Februari 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581231
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


Ubunifu wa 'Royal Tour' ulivyoanza kwa hadhi sumaku inayonasa 'dhahabu watalii'

Baada ya vitambulisho sasa kwenye stika!

BUFE

IJUMAA FEBRUARI 24, 2023 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Mbunge Jafo alipotinga vijijini kukagua kero sugu za miundombinu Kisarawe

ZAMA ZA AWAMU YA SITA...


Ubunifu wa 'Royal Tour' ulivyoanza kwa hadhi sumaku inayonasa 'dhahabu watalii'

• Kuzinduliwa tu, wakala kimataifa wakatua...
• Yaibua bidhaa hewa ukaa iliyoko dukani sasa

Na Mwandishi Wetu

UKURASA 11



## RPC asema maelezo ya mtuhumiwa yatolewe mahakamani

UK. 19



# Mwalimu mbaroni kifo mwanafunzi

• **Adaiwa** kumpiga mateke ubavuni, wazazi wagoma kuzika, Mwenyekiti CCM auawa kwa mapanga... *Ukurasa 2 & 3*



Waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kamsisi, Leonard Mapinda (51), aliyeuawa kwa kukatwa mapanga usiku akiwa amelala nyumbani kwake kwenye kata hiyo wilayani Mlele mkoani Katavi. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

# Benki yataja sababu kurejea tena Tanzania

UK.2



# Zitto autaka urais

UKURASA 3

**MICHEZO** **NABI AWACHARUKIA 'WAZEMBE' YANGA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akihutubia wakati wa ufunguzi wa kwanza wa Jukwaa la Uwekezaji na Biashara baina ya Tanzania na Umoja wa nchi za Ulaya (EU), jijini Dar es Salaam jana, lenye washiriki zaidi ya 800 kutoka nchi zote mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yataja sababu za kurejea Tanzania

**Na Romana Mallya**

BENKI ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (EIB) imeeleza sababu za kurejea Tanzania na kufanya uwekezaji mkubwa wenye thamani ya Euro milioni 540 baada ya kutokuwapo kwa miaka saba nchini.

Moja ya sababu hizo ni maboresho yaliyofanyika na Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo mazingira mazuri ya biashara kwa wawekezaji.

Makamu wa Rais wa EIB, Thomas Ostros aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa Kongamano la Biashara Kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU) lililofunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kwa niaba ya Rais Samia.

Ostros alisema maboresho na mazingira mazuri ya biashara ndiyo yaliyowafanya kurejea Tanzania na leo wanatarajia kutia saini hati ya makubaliano ya fedha hizo.

Pia alisema benki hiyo imerudi Tanzania baada ya UVIKO-19 na kwamba iko tayari kufanya uwekezaji mkubwa wenye thamani ya Euro milioni 540.

Alisema fedha hizo zinatolewa kwa lengo la kuwawezesha wawekezaji na wafanyabiashara wakiwamo wanawake na sekta kama maji, utalii na kampuni zinazojihusisha na uchumi wa bluu.

"Hii itafanyika kupitia ushirikiano na kifedha kati ya EIB na benki za CRDB, NMB, na KCB pamoja na makubaliano yaliyofanyika leo (jana) kati ya Kampuni ya Umoja wa Ulaya na Tanzania, kampuni za Tanzania zitakazowawezesha kuwekeza na kupanua biashara zao hususani katika utalii na uvuvi," alisema.

Katika kongamano hilo, Makamu wa Rais, Dk. Mpango, alishuhudia utiaji saini wa hati tatu ikiwamo ya Huduma ya Usafiri wa Anga iliyotiwa saini na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbalawa na Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Uchumi wa Ufaransa, Olivier Becht.

Lengo lake ni kuongeza safari za ndege za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam kwenda Kisiwa cha Mayotte, Ufaransa ifikapo mwezi Juni mwaka huu. Nyingine ni kati ya Bandari ya Antwerp-Bruges International na Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA) ambayo itaongeza usimamizi wake na kuimarisha miundombinu ikiwamo bandari kavu na bandari za maziwa.

Hati ya makubaliano ya tatu inahusisha ujenzi wa mradi wa uzalishaji wa umeme wa Kakono Hydro Power utakaojengwa mkoani Kagera uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo Afrika chini ya ufadhili wa EU.

Akizungumza kwenye kongamano hilo la siku mbili lililohudhuriwa na washiriki 800 wakiwamo wawekezaji 270 kutoka nchi 27 za EU, Dk. Mpango aliwataka wawekezaji hao kuja kuwekeza kwenye maeneo yanayoendana na mahitaji.

Alisema lengo ni kuiwezesha Tanzania kutimiza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na kutoka uchumi wa kati wa chini hadi uchumi wa kati wa katikati.

Alitaja vipaumbele vya nchi kwenye uwekezaji ni katika sekta ya kilimo, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo, viwanda vya dawa na vifaa tiba, ujenzi, sayansi, teknolojia, maendeleo ya viwanda katika kizazi cha nne.

"Serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara kwa kuendelea kurekebisha sheria.

"Kuboresha mifumo ya ulipaji kodi ikiwamo sera za ulipaji kodi kwa nchi kumi, kuimarisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)," alisema.

Makamu wa Rais pia alisema wanalenga kuimarisha upatikanaji wa umeme, uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, Bandari kavu ya Kwala, ujenzi wa barabara na reli na uanzishaji wa Sheria ya Uwekezaji ya 2022 ikifuta ile ya 1997.

Kadhalika, alisema jukwaa hilo linapaswa kuwa chachu ya kuongeza uwekezaji wa Umoja wa Ulaya nchini na kuwa sehemu ya kujenga imani na uaminifu kwa pande zote mbili.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji alisema kupitia kongamano hilo, Tanzania inatarajia kulifikia soko la nchi za EU lenye zaidi ya watu milioni 400.

Waziri wa Biashara na Vivutio vya Uchumi wa Ufaransa, Olivier Becht katika hotuba yake, aliahinisha nia ya Ufaransa ya kuimarisha uwekezaji Tanzania hususan sekta za kimkakati.

Pia alisema ushirikiano baina ya nchi hizo una tija kutokana na Tanzania kuwa nchi inayokua kwa haraka kiuchumi hivi sasa.

Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Manfredo Fanti aliitaja siku ya jana kuwa maalum kati ya Tanzania na EU.

Katika mkutano huo, wawekezaji hao walionyeshwa video fupi ikihusisha uwekezaji mkubwa uliofanywa na mwekezaji ambaye ni kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania iliyoko Kisemvule, Mkuranga mkoani Pwani ambayo imepanga kupanua uzalishaji wake.

# Mwalimu mbaroni kifo cha mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

UTATA umeibuka kuhusu kifo cha mwanafunzi wa kidato cha nne wa shule ya sekondari iliyoko Pasua, Manispaa ya Moshi, Walter Ebenezer, anayedaiwa kushambuliwa kwa mateke kwenye mbavu na mwalimu wake kisha kupewa adhabu ya kupiga 'push up'.

Kutokana na kifo hicho, ndugu wa mwanafunzi huyo wamejitokeza hadharani wakiliomba Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro kufanya uchunguzi wa kitabibu kubaini sababu za kifo hicho.

Inadaiwa kuwa mwanafunzi huyo kabla ya kupoteza maisha Februari 19 mwaka huu kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru) alikokuwa anapatiwa matibabu, alikuwa mwanafunzi wa bweni wa shule hiyo.

Akizungumzia tukio hilo jana, mama mdogo wa marehemu, Mkazi wa Sakina-Arusha, aliyejitambulisha kwa jina moja la Neema, alidai kuwa kabla mwanafunzi huyo hajafariki dunia, aliwaambia kwamba alipigwa na mwalimu wake mateke kwenye mbavu na aliambiwa apige push up kutokana na kosa ambalo hakuliweka wazi. "Baba mzazi wa marehemu, alipigiwa simu akaambiwa akamchukue mtoto maana anaumwa sana. Alipokwenda shuleni kumchukua mtoto, alimleta Mount Meru kwa ajili ya matibabu.

"Alipofikishwa Mount Meru, alipatiwa matibabu na aliwekewa oksijeni. Baadaye mtoto alipoteza maisha. Lakini tulikwenda kufuatilia polisi. Tulianzia Central Arusha (Kituo Kikuu cha Polisi) na baadaye tukaelekezwa twende Central ya Moshi mahali ambako tukio ndiko lilitokea. "Tulimwelezea OCD Moshi (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) tukio zima na akachukua gari na askari na wakaenda shuleni, hawakumpata mwalimu, wakaambiwa warudi siku iliyofuata.

"Niliwauliza polisi kama tunaruhusiwa kuzika mwili, nikaambiwa 'hapana!', tunatakiwa kusubiri mpaka wafanye uchunguzi wao," alidai. Hata hivyo, mama mdogo wa mwanafunzi huyo aliendelea kudai kuwa walipokwenda Kituo Kikuu cha Polisi Arusha, waliambiwa wanatakiwa wauzike mwili huo.

"Tunashangaa tutazikaje wakati Central Moshi wametuzuia na ndio ambako tukio limetokea? Tunazikaje huo mwili, mbona wanafamilia tunachanganywa? Tunazikaje wakati hatujajua mwafaka wa ndugu yetu amekufakufaje? Tunahitaji haki, uchunguzi ufanyike," alisisitiza.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alikiri jeshi hilo linamshikilia mmoja wa walimu wa shule hiyo (hakumtaja jina) kwa ajili ya uchunguzi. "Tumefungua jalada la uchunguzi. Kwa sababu ni malalamiko, ni jukumu letu kumshikilia ili tujiridhishe. Timu yangu ya makachero imekwenda kufanya postmortem (uchunguzi wa kitabibu) ili tujiridhishe kwamba ni kweli aliuawa au alikuwa anaumwa?

"Tunachunguza lakini hatuwezi kusema moja kwa moja. Sasa kumshikilia ni jukumu letu, kwa sababu kuna malalamiko juu yake. Tunasubiri madaktari, watuambie kwamba chanzo cha kifo chake ni nini.

"Makachero wetu wamekwenda huko (Hospitali ya Mount Meru) kujiridhisha kwanza na hiyo taarifa, kama kweli ipo na kama ipo, basi washirikiane na ndugu ili 'ku-clear' (kumaliza) hiyo doubt (shaka). Bado uchunguzi unaendelea, tunamshikilia kwa ajili ya uchunguzi na sio kwa sababu ya mauaji," alisema.

# Zitto autaka urais

**Na Mwandishi wetu**

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe amesema dhamira yake kubwa ya kuwa kwenye ulingo wa siasa ni kuwa Rais wa Tanzania atakayeibadilisha nchi pale ilipo na kupiga hatua kubwa kimaendeleo.

Zitto alitoa kauli hiyo jana Dar es Salaam alipohojiwa katika kipindi cha Super Breakfast kinachorushwa na Kituo cha Redio cha East Africa ingawa hakutaja kama atagombea nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu ujao wa 2025.

Alisema dhamira yake kuu kama mwanasiasa ni kuona siku moja anakuwa Rais wa Tanzania kupitia mifumo halali ya kiuchaguzi na kwamba ukaribu wake na baadhi ya mawaziri wanaotokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM), una lengo la kupanga safu ya uongozi kwa ajili ya uchaguzi wa 2025.

"Tunajenga chama ili siku moja kije kushika dola na kila mwanasiasa dhamira yake kuu ni kushika nafasi ya juu kabisa ya kisiasa inayotokana na mifumo ya kisiasa na nafasi hiyo ni urais na mimi ninautaka urais," alisema Zitto.



Aliongeza kuwa kwa sasa yeye ni kiongozi mwenye jukumu la kuhakikisha chama chake kinapiga hatua ya kimaendeleo, ikiwamo kuongeza wanachama kusimamia sera za chama na kuhakikisha anakabidhi majukumu hayo kwa kiongozi atakayekuja badala yake.

"Mwezi wa tatu (Machi) mwakani mimi nitang'atuka katika uongozi wa chama, nitakuwa nimeshatumia mihula miwili ya uongozi kwenye nafasi hiyo, nitawaachia wenzangu watakaochaguliwa kuongoza lakini dhamira yangu ya siku moja kuwa Rais wa Tanzania itabaki pale pale," alisisitiza Zitto.

**MIKUTANO YA HADHARA**

Akizungumzia nafasi ya vyama vya siasa baada ya kuondolewa kwa zuio la mikutano lililodumu kwa takriban miaka saba, Zitto alisema mfumo wa demokrasia ulirudishwa nyuma kwa miaka 30 wakati kulipokuwa na chama kimoja na kwamba sasa vyama vya siasa vina kazi ya kujijenga upya katika maeneo mbalimbali nchini.

Zitto alisema moja ya vitu walivyopigania kwenye kikosi kazi ni kuwapo Katiba Mpya, jambo ambalo kwa sasa limezungumzwa na karibu kila chama.

Alisema kuwa wakiwa kwenye kikosi kazi, walitaka mikutano ya hadhara iruhusiwe, mchakato wa Katiba Mpya ufanyike ikiwa ni pamoja na uandishi wa sheria mpya ya vyama vya siasa na ya uchaguzi.

Alieleza kuwa baadhi ya watu wanaosema Katiba haileti chakula, ni watu wa kupuuzwa kwa kuwa kila kinachofanyika nchini kinahusisha katiba, hivyo kuiepuka ni jambo lisilowezekana.

# Mwenyekiti wa CCM auawa kwa mapanga

**Na Neema Hussein,** MLELE

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Kamsisi, Halmashauri ya Mlele mkoani Katavi, Leonard Mapinda (51), ameuawa kwa kukatwa mapanga usiku akiwa amelala ndani ya nyumba yake.

Tukio hilo limefanywa usiku wa manane na watu ambao hawajafahamika, ikidaiwa kuwa kabla hawajatekeleza tukio hilo, walimtaka kiongozi huyo kutoa fedha alizokuwa nazo.

Akizungumza baada ya kuuaga mwili wa mwenyekiti huyo, Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Majid Mwanga aliwataka wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kuwabaini waliotekeleza mauaji hayo.

Pia aliagiza kukamatwa vijana wote wanaozurura mitaani bila kazi kwamba huenda wanawafahamu waliofanya mauaji hayo.

"Ndugu zangu, waombolezaji wenzangu, nilisema jana na ninayarudia leo, hawa wahalifu wanaotaka kujenga chuki, tushirikiane na Jeshi la Polisi kuwasaka usiku na mchana.

"Kamata vijana ambao wanacheza pool table ovyo, wanaocheza kamari, kamata walevi ambao wanakaa vilabuni, kamata wote hao watakwambia ni nani aliyefanya hivyo, tuko hapa kwa ajili ya kusimamia ulinzi wa wananchi wetu, lakini tunawasindikiza wengine wanaokwenda mahabusu, ninajua wamejaa hapa wanaojua nani amefanya jambo hili, tunafahamu ulipo tupo," alisema Mwanga.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Songambele, Peter Manyandodi alisema matukio hayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara kijijini huko na kuwataka wananchi kuyachunguza vizuri ili waisaidie serikali kuchukua hatua.

Diwani wa Songambele, Leonard Kiyungi aliwataka wananchi kutojichukulia sheria mkononi na kufuata utaratibu wa kisheria.

"Kwa kweli tabia kama hii wananchi wa Songambele ninaomba tuachane kabisa, serikali imetuwekea utaratibu mzuri, imetuwekea watendaji wa vijiji, watendaji wa kata, imetuletea Jeshi la Polisi, imetuletea mahakama, hivyo vyote vyombo vya dola vipo kwa ajili ya kutatua changamoto zetu," alisema diwani huyo.

Filimina Katoto, Diwani wa Viti Maalumu Songambele, aliwataka wananchi wanapopokea wageni kwenye nyumba zao, watoe taarifa kwa uongozi wa serikali za mitaa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# TANGAZO KWA UMMA

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), kwa kushirikiana na Mtaalam Mshauri wa Fidia (NORPLAN (T) Ltd), inatarajia kuendesha zoezi la kuhakiki taarifa za uthamini wa fidia kwa watu wanaoathirika na utekelezaji wa **Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Msimbazi.** Uthamini ulifanyika mapema mwaka 2022 katika maeneo yote yanayoathirika na mafuriko katika Bonde la Mto Msimbazi na waathirika walipewa namba za uthamini.

Ili kufanikisha zoezi la uhakiki, watu wote waliotambuliwa na kupata namba za uthamini, watatakiwa kufika katika ukumbi wa **DRIMP (Ilala Kota)** kuanzia **tarehe 06** hadi **11/03/2023** (saa **3:00 asubuhi**) ili kuhakiki taarifa zao na kusaini nyaraka husika. Waathirika watafika kwa utaratibu wa mitaa yao, kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Tarehe | Mitaa Husika |
|---|---|---|
| 1 | 06hadi 07, Machi 2023 | Suna<br>Hananasif<br>Idirisa<br>Mkunguni A |
| 2 | 08 hadi 09, Machi 2023 | Kigogo Mbuyuni<br>Mkunguni B<br>Mtambani<br>Kawawa<br>Charambe<br>Ilala Kota<br>Kariakoo Kaskazini<br>Jangwani |
| 3 | 10 hadi 11 , Machi 2023 | Misheni Kota<br>Msimbazi bondeni<br>Mtambani A<br>Mtambani B<br>Mwinyi Mkuu |

Mara uonapo tangazo hili, tafadhali mfahamishe na mwenzako ili aweze kufika bila kukosa kwa kadiri ratiba inavyoelekeza.

**KATIBU MKUU**
**OR-TAMISEMI**




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Ruge Mutahaba Foundation, Cynthia Bavo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kabla ya kikao cha wadau mbalimbali kitakachojadili kutafuta suluhu bunifu na endelevu kwa ukosefu wa ajira kwa vijana. Kushoto ni Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa taasisi hiyo, John Ulanga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jela miaka 20 uhujumu uchumi

**Na Halima Ikunji,**
TABORA

JUMANNE Kulwa Sizya (31), mkazi wa Kata ya Ipole, Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, amehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela baada ya kutiwa hatiani kwa makosa manne ya uhujumu uchumi.

Akitoa hukumu hiyo juzi, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Tabora, Sigwa Mzige alisema mahakama hiyo imefikia hatua hiyo baada ya mtuhumiwa Sizya kukutwa na hatia katika makosa manne ambayo ni; kuingia kwenye hifadhi bila kibali, kupatikana na silaha, kukutwa na nyara za serikali, kupatikana na silaha za mlipuko pamoja na kujenga kambi hifadhini.

Alisema mshtakiwa huyo alikamatwa na maofisa wa wanyamapori kwenye Kijiji cha Isimbila, kwenye Hifadhi ya Ugalla wilayani humo na alipopekuliwa, hakuwa na kibali chochote ambacho kinamruhusu kuingia hifadhini.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo kutokana na mshtakiwa kuthibitika kutenda makosa hayo ambayo yamemtia hatiani, ikieleza kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria ya nchi.

Wakili wa Serikali Lucy Kyusa alidai mahakama huko kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo mnamo April 12, 2022 kwenye eneo la Isimbila, ndani ya Hifadhi ya Ugalla wilayani Sikonge mkoani Tabora.

Hakimu Mzige alisema mshtakiwa huyo katika kosa la kwanza alitakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela mwaka mmoja. Kwa kosa la pili hadi la nne, amepewa adhabu ya kwenda jela miaka 20.

"Mahakama hii inazingatia makosa aliyotenda mshtakiwa Jumanne Kulwa ya kuhujumu uchumi, ni kosa la kuingia kwenye hifadhi bila ya kuwa na kibali na kukutwa na silaha za moto, serikali hairuhusu," alisema.

Wakitoa ushahidi mahakamani huko, maofisa wa wanyamapori walidai walipofanya doria kwenye hifadhi hiyo kwa kufuata nyayo za baiskeli, walimkuta mshtakiwa akiwa ameweka kambi na walifanikiwa kumkamata hifadhini.

Mshtakiwa Kulwa katika utetezi wake alikana kukamatwa hifadhini na maofisa hao na kudai mahakamani kuwa alikuwa anatokea shambani kulima na alikuwa na jembe mkononi mwake huku akiomba mahakama kumpunguzia adhabu kutokana na kwamba ana mke mmoja na watoto wawili wanaosoma.

Licha ya utetezi huo, mshtakiwa huyo alikuhumiwa kutumikia miaka 20 gerezani.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

### TANGAZO LA FURSA ZA MAFUNZO YA UANAGENZI KWA VIJANA

1. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini inayolenga kuwezesha nguvu kazi ya Taifa kupata ujuzi na stadi za kazi stahiki ili kumudu ushindani katika soko la ajira. Ofisi imeingia makubaliano na vyuo 28 ya kutoa mafunzo katika fani mbalimbali zikijumuisha: Ubunifu wa Mitindo na Ushonaji Nguo, Ufundi Bomba, Uashi, Useremala, Uchomeleaji na Uungaji Vyuma, Uchoraji na Maandishi ya Alama, Utengenezaji wa Vipuri vya Mitambo, Kuongoza Watalii, Ufundi Magari na Mitambo, Umeme wa Majumbani na Viwandani, TEHAMA, Umeme wa Magari, na Huduma za Hoteli na Utalii.

2. Hivyo, tunapenda kuwatangazia vijana wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 wanaopenda kujiunga na mafunzo katika mojawapo ya fani zilizoorodheshwa hapo juu wafike katika vyuo vilivyoainishwa na Tangazo hili hapa chini ili kuchukua fomu ya kuomba kujiunga na mafunzo. Serikali itafadhili ada ya mafunzo kwa asilimia 100. Mwanafunzi / mzazi / mlezi atagharamia gharama nyingine zikijumuisha nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani. Mafunzo yatakua ya kutwa hivyo muombaji anashauriwa kuomba mafunzo haya katika chuo kilicho katika Mkoa anaoishi.

3. Maombi yawasilishwe kuanzia tarehe 27/02/2023 hadi tarehe 10/03/2023 yakiambatana na nyaraka zifuatazo:
   i. Barua ya maombi ya mafunzo;
   ii. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa;
   iii. Nakala ya Cheti cha elimu uliyohitimu ;
   iv. Kitambulisho cha uraia / kadi ya mpiga kura (Kwa wenye miaka 18 na kuendelea);
   v. Barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji anakoishi mwombaji; na
   vi. Picha nne za paspoti (ziandikwe majina matatu ya mwombaji kwa nyuma).

4. Sifa za kujiunga na mafunzo haya ni:
   i. Elimu ya msingi au zaidi kwa fani za ubunifu wa mitindo na ushonaji nguo, ufundi bomba, ujenzi, useremala, uchomeleaji na uungaji vyuma, upakaji rangi na maandishi ya alama;
   ii. Elimu ya kidato cha nne na kuendelea kwa fani nyingine zilizobaki zikijumuisha fani ya utengenezaji wa vipuri vya mitambo, umeme wa majumbani na viwandani, TEHAMA, na umeme wa magari;
   iii. Awe Mtanzania;
   iv. Awe na umri kati ya miaka 15 – 35;
   v. Awe mwenye afya njema.

5. Vijana wa Kike na Vijana Wenye Ulemavu wanasisitizwa kuomba fursa hizi na watapewa kipaumbele katika nafasi za mafunzo haya;

6. Maombi yachukuliwe na kuwasilishwa kwenye vyuo vilivyo karibu katika Mkoa wako ambavyo vimekubaliwa na Serikali kutoa mafunzo haya; na

7. Watakaokidhi vigezo na sifa tu ndio watakaochaguliwa.

Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Ofisi **(www.kazi.go.tz)**

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MKUU**
**22/02/2023**

NB: Fomu za maombi zinapatikana katika vyuo vyote vilivyopitishwa na Serikali kutoa mafunzo haya.

# Taasisi ya Ruge Mutahaba kuwafikia vijana 100,000

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Ruge Mutahaba Foundation imesema katika mpango kazi wake wa miaka mitano imepanga kuwafikia vijana 100,000, ili kuwawezesha kutumia fursa na ubunifu kupata suluhisho la tatizo la ajira.

Mtendaji Mkuu wa Ruge Mutahaba Foundation, Cynthia Bavo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa wadau wanaojihusisha na masuala ya kusaidia vijana na uchumi waliokutana kujadili namna ya kulisaidia kundi hilo kwenye eneo la ajira na kazi.

Mkutano huo ambao umeandaliwa na taasisi hiyo, umefanyika ikiwa ni miaka minne tangu kufariki dunia kwa Ruge ambaye enzi za uhai wake, aliwekeza katika ubunifu na ujasiriamali wa vijana na wanawake kwa kuwasaidia katika kuinua kipato.

Akizungumza katika mkutano huo, Bavo alisema wamekutana na wadau hao, ili kuweza kujadili namna ya kusaidia vijana ambao kwa sasa walio wengi hawana ajira.

"Kama taasisi zisizo za kiserikali na taasisi nyingine tofauti tumekutana ili kuangalia hii shida ya vijana ya kutopata kazi na kuitatua, namna ya kutatua ni kufanya kazi na wadau tofauti, kwenye kuwezesha vijana kupata kazi, kuweza kuanzisha biashara hatuwezi kufanya wenyewe," alisema.

Pia alisema wataangalia namna vijana watakavyoweza kuzifikia kazi kwenye mitandao na kuangalia sekta rasmi na namna ambavyo watasaidia kutengeneza kazi zaidi.

Kadhalika, alisema wataangalia sekta isiyo rasmi kwa wale wanaokosa kazi kuwasaidia kuingia sekta rasmi.

Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa taasisi hiyo, John Ulanga akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wake, Prof. Rwekaza Mukandala alisema watashirikiana na wadau kutengeneza majawabu kuhusu tatizo la ukosefu wa ajira. "Huwezi kutengeneza majawabu peke yako, ni lazima mkae kwa pamoja ili kuweza kutafuta ufumbuzi, mfano suala la kujiamini, kutambua vipaji na kukifanya kuwa ajira, ubunifu na kuhakikisha zinazaa manufaa, kuhakikisha vijana wanakaa pamoja badala ya kulalamika waangalie fursa," alisema.

Alisema watakuwa wakitoa mchango wao kama wadau wengine wanavyofanya ili utumike kutatua tatizo hilo.

"Hapa Tanzania karibu kila mwaka kuna vijana wapatao milioni moja wanaingia kwenye soko la ajira na haiwezekani sekta rasmi ikawachukua wote, ni ukweli kwamba asilimia kubwa ya ajira ama zinatolewa kwenye sekta isiyo rasmi au sekta ndogo ndogo," alisema.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuwaweka wadau wote pamoja ili kupanga mikakati ambayo itasaidia taasisi kupanga mpango kazi. Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Tanzania Startup, Zahoro Muwaji alisema ni lazima watu watambue kuwa kuna tofauti kati ya ajira na kazi.

"Ajira ni chache, kazi ni nyingi na vijana wengi sasa wanatafuta kazi kwa maana kwamba ni vitu wanavyoweza kuvifanya wao wenyewe bila kuajiriwa, vijana wengi kwa sasa wanatengeneza maudhui na kuweka mtandaoni na kupata kipato," alisema.

Muwaji alisema ni vyema kwa taasisi ya Ruge kuangalia zaidi mazingira ya uwezeshwaji, ili kuchochea watu kufanya ubunifu na kuzalisha maudhui na bidhaa ambazo watauiuza popote.

# Waliojitambulisha kuwa usalama wa taifa wakutwa na kesi kujibu

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewakuta wana kesi ya kujibu, washtakiwa wawili wanaodaiwa kujitambulisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu kwamba ni maofisa kutoka Ofisi ya Rais, Idara ya Usalama wa Taifa.

Washtakiwa hao, Joshua Kamalamo na Yahaya Kaparatu, walikutwa na kesi ya kujibu jana mahakamani hapo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate.

"Kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka, mahakama inaona kuna haja ya washtakiwa kutoa utetezi wao," alisema Hakimu Kabate katika uamuzi wake. Baada ya kutoa uamuzi huo, shauri hilo liliahirishwa hadi Machi 28, mwaka huu, washtakiwa watakapoanza kujitetea dhidi ya shtaka linalowakabili.

Upande wa mashtaka katika shauri hilo, ulikuwa na mashahidi wanne akiwamo DPP na vielelezo viwili.Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo Juni 12, 2021, katika ofisi za DPP zilizoko ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, mtaa wa Ohio, Dar es Salaam.

Kamalamo anadaiwa alimweleza DPP kuwa kituo chake cha kazi ni Makumbusho na Kaparatu alidai alipandikizwa katika ofisi za kampuni ya PAP inayomilikiwa na Mfanyabiashara Habinder Seth Singh.

Inadaiwa walikwenda kwa DPP kumpa maelekezo kutoka Ikulu ya kwamba asitishe mchakato wa majadiliano ya kumaliza kesi ya uhujumu uchumi namba 27 ya mwaka 2017, iliyokuwa inamkabili Seth na wenzake mpaka watakapompa maelekezo mengine.

Inadaiwa walitoa sababu kuwa wao wanajua vitu vingi kuhusu Seth, hivyo yeye afuate maelekezo hayo jambo ambalo alilitilia shaka na kuamua kufanya mawasiliano na idara ya sheria Ikulu kwa njia ya simu.

Baada ya mawasiliano hayo, ilidaiwa kuwa Mwakitalu alipewa majibu kuwa hakuna maagizo ya namna hiyo wala idara hiyo haina maofisa wenye majina hayo.

# Mkemia: Siyo kila sumu inaondolewa kwa maziwa

Na Mary Geofrey

MAMLAKA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imewatahadharisha wananchi kuwa makini na matumizi ya maziwa katika kuondoa sumu mwili.

Mratibu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu wa GCLA, Yohana Goshashy, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mafunzo ya kuwajengea uelewa watoa huduma za afya ngazi ya jamii kuhusu namna ya kudhibiti sumu.

Alisema wananchi hawana uelewa kuwa kuna aina tofauti za sumu ambazo nyingine zinaondolewa kwa maji kama maziwa na ambazo hazitakiwi kukutana na maji. "Maziwa siyo kiua sumu kwa yule ambaye amekunywa au kunyweshwa sumu ambayo haiitaji maji kuingia mwilini, hivyo inaweza kumwongozea tatizo, lakini yanaweza kumsaidia yule ambaye sumu aliyotumia inaondoka kwa kunywa maji," alisema Goshashy.

Aidha, alionya wale ambao wanapenda kuondoa sumu za nyoka kwa kuchanja juu ya jeraha kwa sababu kuna sumu nyingine zinasababisha damu kuyeyuka, hivyo kumfanya mgonjwa kutokwa na damu nyingi.

"Kuna nyoka wengine ukichanja juu ya jeraha maana yake umesababisha madhara yawe makubwa, mfano kuna wale nyoka ambao wanasumu inayosababisha damu isigande mwilini hivyo ukichanja unasababisha damu imwagike kwa wingi," alisema.

Goshashy alisema kufunga mguu juu ya jeraha, inatakiwa upate ushauri wa namna ya kufunga kwa sababu zipo sumu ambazo zinashambulia mishipa ya fahamu na madhara kuwa makubwa.

"Kuliko ufunge bora upige simu kituo cha kudhibiti matukio ya sumu au kituo cha afya kilicho karibu wakushauri namna ya kufunga kwa kuruhusu damu iendelee kupita," alifafanua Goshashy. Alishauri watu wanaopata matukio ya sumu watoe taarifa katika kituo cha afya kilicho karibu au kupiga simu kituo cha matukio ya sumu kwa namba 0736623333.

Alisema wametoa mafunzo kwa watoa huduma za afya ngazi ya jamii katika Manispaa yote ya Ilala na matarajio ni kufikia wilaya zote za mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu kundi hilo linakutana na wananchi moja kwa moja.

Naye Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, aliwataka watoa huduma hizo kutumia elimu waliyopata kusaidia kuelimisha jamii na kupunguza matukio ya simu kwa jamii.

Alisema GCLA itaendelea kushirikiana na jamii katika kufikisha elimu ili kupunguza madhara yatokanayo na sumu.

Naye mtoa huduma za afya ngazi ya jamii, kata ya Mnyamani, Mambo Mdadike, alisema mafunzo hayo yana tija kwa sababu kama watoa huduma za afya walikuwa hawana uelewa nayo.

"Mengine tulikuwa hatuyafahamu, naamini kupitia mafunzo haya nasi sasa tutaelimisha jamii, ikitokea tumekutana na mtu aliyekunywa sumu au kuumwa na nyoka, tunajua tumsaidiaje," alisema Mdadike.


SALAMU ZA PONGEZI

ACB
AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako




Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Akiba Commercial Bank Plc wanatoa pongezi zao za dhati kwa Bi. Etness Chanza kwa kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Malawi na Mhe. Dkt. Lazarus. Mc Carthy Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi. Tunamtakia kila la kheri anapoachia nafasi yake kwenye bodi ya ACB na kuanza majukumu yake mapya ambapo tuna imani kwamba ujuzi na uzoefu wake utakuwa wa manufaa makubwa kwa Mahakama ya Malawi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utabiri TMA kuhusu mvua uchukuliwe kwa tahadhari

**MAMLAKA** ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), juzi ilitoa utabiri unaoonyesha kuwa katika baadhi ya mikoa kunatarajiwa kunyesha mvua kubwa ambayo huenda ikasababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, maeneo ambayo yanatarajiwa kuwa na mvua kubwa ni Dar es Salaam, Morogoro, Pwani na visiwa vya Unguja na Mafia.

Utabiri huo unaonyesha kuwa baadhi ya mikoa inatarajiwa kuwa na mvua za wastani. Mikoa hiyo ni ya kanda ya Kaskazini (Arusha, Tanga Kilimanjaro na Manyara), Kanda ya Ziwa (Mwanza Shinyanga, Simiyu, Mara na Geita) pamoja na kaskazini mwa Kigoma.

Kutokana na utabiri huo, ni wazi kwamba mikoa ambayo inatarajiwa kupata mvua nyingi, inaweza kupata madhara yakiwamo mafuriko na hata uharibifu wa mali. Kwa upande wa ile itakayopata mvua za wastani, TMA imesema inaweza kukumbana na uhaba wa unyevu kwenye udongo, hivyo kushindwa kustawisha baadhi ya mazao hasa yale yanayohitaji unyevunyevu wa kutoksha kwa ajili ya mazao hayo.

Utabiri huu wa TMA umetolewa kwa wakati kwa kuwa unaonyesha kuwa hali hiyo ya hewa inatarajiwa kujitokeza mwezi ujao, hivyo kuna nafasi kwa maeneo husika kuweka mipango thabiti kukabiliana na hali hiyo. Kwa mantiki hiyo kila eneo ambalo linaguswa na utabiri huo, linapaswa kuchukua hatua zinazostahili na kama ilivyoshauriwa na mamlaka.

Kwa mikoa ile ambayo imetajwa kuwa na mvua za wastani, inapaswa kujizatiti kupitia maofisa ugani kuhakikisha wananchi wanazalisha mazao yanayostahili mvua za wastani pamoja na yale yanayostahili ukame ili kuwa na uhakika wa chakula siku za baadaye.

Mikoa ambayo imetajwa kuwa na mvua kubwa, Dar es Salaam ikiwamo, inapaswa kuchukua tahadhari kubwa kwa sababu kunaweza kutokea uharibifu wa mali na miundombinu ya umma kama vile barabara na matokeo yake hali ya usafiri kuwa ngumu kwa baadhi ya sehemu.


Ni wazi kwamba katika mkoa wa Dar es Salaam inaponyesha mvua, baadhi ya sehemu hukumbwa na matatizo kama vile nyumba kubomoka kwa zile zilizojengwa chini ya viwango na zilizoko mabondeni, maji kujaa na kusababisha mafuriko katika sehemu ambazo miundombinu ya kusafirisha maji ya mvua na mifereji ya maji machafu huziba na kushindwa kupeleka uchafu kunakohusika.

Kama TMA ilivyoshauri, ni vyema serikali na mamlaka za serikali za mitaa katika mkoa wa Dar es Salaam, zikachukua hatua zinazotakiwa kama vile kuzibua mifereji ya maji machafu, kuondoa takataka kwenye mito ili kuruhusu maji kupita bila matatizo na usafiri kuwa na uhakika wakati wote.

Jambo hilo ni la muhimu kwa sababu hivi karibuni, mvua iliyonyesha kwa takriban saa nane, ilisababisha matatizo katika baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam. Mvua iliyotangazwa kuwa itanyesha kwa mujibu wa TMA, inatarajiwa kunyesha kwa kipindi kirefu na kwa mfululizo wa saa kadhaa kwa wakati, hivyo ni dhahiri kwamba inaweza kusababisha matatizo zaidi ya yale ya mvua ya muda mfupi iliyonyesha hivi karibuni.

Wahenga wanasema tahadhari kabla ya hatari. Kwa mantiki hiyo, hatua za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kukabiliana na mvua zinazotarajiwa kunyesha kuanzia mwezo ujao. Kwa kufanya hivyo, maana yake ni kwamba mvua hizo hazitasababisha madhara kama yale ambayo yamekuwa yakijitokeza kila mwaka pindi mvua zinaponyesha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hizi juisi za mtaani, zinatuweka njia panda kuhusu usalama wa afya zetu

Na Yasmine Protace

**NI** jambo la kawaida sana katika jamii, kinywaji juisi inashika nafasi kubwa zaidi kwa namna yoyote ile.

Inaweza kuwa katika sura ya starehe, pia hata sababu za kiafya, bado juisi inahitajika.

Msingi wa juisi ni tunda lililoloko katika mfumo wa kinywaji, maji ikiwa ni sehemu yake. Ni jibu lilile bayana, mtu akiingia kwenye nyumba ya mtu na hasa mijini, akafungua friji, si ajabu kukuta juisi.

Manufaa au uzuri wa juisi ina sura mbili, burudani inayopatikana hadi baa, vilevile kuna suala la afya kuongeza matunda mwili.

Mpaka sasa huwezi kuingia kwenye duka ya sehemu nyingine ya mauzo ya vyakula, kawaida lazima utakuta juisi. Hiyo inatokana na kushamiri biashara hiyo, kila unakoenda huwezi kukosa juisi.

Hapo kuna harakati za kijasiriamali ambazo, daima hutumia mapengo yanayojitokeza kuwekeza mauzo ya bidhaa wanazozalisha na kuziweka sokoni, juisi ni mojawapo.

Kwa walaji kwetu, napo tunakuta nafuu, kwani kuna baadhi yetu tunajaribu kujitenga na kutumia sana vitu vya viwandani, kama hizo juisi nilizozisema. Wanapopita wajasiriamali wa kawaida wa juisi, tunaangukia kwao, vilevile kwa bei za juisi zao napo si haba kwetu!

Niangukie kwingine shida ya kizuri hakikosi kasoro. Je vina kasoro? Ukweli upo kwamba kuna kasoro kubwa, kutoka kwa tabia binafsi ya wauzaji kwenye kiafya na kutunza miili yao, hata kuangukia kwenye bidhaa zao na salamu zinaishia kwa mlaji kula uchafu.

Tunakiri kwamba, biashara hiyo ya juisi mitaani inamuingizia kiasi cha mapato mzalishaji na muuzaji akijikimu au kunufaika kwa namna anavyojua yeye kiuchumi.

Lakini, siku zote kuna angalizo mahsusi likiwataka wafanyabiashara kujali afya za wateja wao, dhidi ya tabia kutumia chupa na kisha baadae, chupa hiyo hiyo ikatumiwa na mteja mwingine.

Nikirejea sasa, ni msimu wa matunda ambao katika baadhi ya masoko kumesheheni ya aina mbalimbali yanauzwa, katika miji yote nchini.

Hapo ndipo penye mwanzo wa angalizo la kiafya, kwamba sote tunapaswa kujali afya za wanywaji juisi hiyo, ili baadae kusiwapo malalamiko kutoka kwa mteja.

Ukweli ni kwamba, kuna chupa zinauzwa madukani, ambako mtu anatumia na kisha kuitupa, au unaweza kutumia glasi na akiosha kwa usafi unaokidhi kiwango, na tukitumia uzoefu wa kinamama, hilo hatuhitaji kufunzana. Lakini, linapokuja hilo la kuokota chupa na kuwawekea watu juisi katika uchafu wake uleule, daima haipo sawa.

Kuna matunda kama vile ndizi mbivu, nanasi, matikiti na maembe, wafanyabiashara wadogo sasa wameibuka na kuzitengenezea juisi wanazozuza, katika maeneo kama vituo vya mabasi hasa mijini, kupitisha majumbani, wengine wakitembeza mitaani na shuleni wakiziuza.

Licha ya kuwapo ukweli ni fursa kwa kila mwekezaji kufanya biashara ya kuuza juisi kusaka kipato, ila msingi wa msiamiati wa 'vigezo na masharti kuzingatiwa' na hasa katika kipengele kanuni afya an usafi.

Kwa sasa, baadhi ya masoko wana mashine za kutengenezea juisi ambako mtu akinunua matunda anapeleka kwa wenye mashine na kusagiwa, na wanahamia katika jukumu la kutembeza mitaani.

Nimkumbushe kila mtu, kwamba juisi inahitaji usafi wa hali ya juu. Changamoto tunayoiona wengi ni kwamba, zinaandaliwa bila ya kuwapo maji yaliyochemshwa.

Kitendo pekee cha kutochemsha maji, kinaweza kusababisha wanywaji kuanza kuumwa matumbo.

Baadhi ya wauza juisi, wanakiuka kanuni hiyo ya kiafya, wakienda mbali sokoni, badala ya kuwa na glasi mahsusi ya kazi hiyo, wanatumia chupa za aina mbalimbali kuuza juisi hiyo.

Tukiangalia chupa mara nyingi unakuta imetumika, halafu watoto wanaziokota na kuzipeleka kwa wauza juisi na wao huweka juisi na kuziuza. Hapo jamani, hatuwezi kusababishia watumiaji juisi matatizo ya kuumwa?

Kinachotakiwa kwa wauza juisi, nyenzo sahihi kama glasi za 'take away' kwa ajili ya kufanyia biashara na sio kuokota chupa na kuweka juisi.

# Serikali yafafanua gharama MV Magogoni

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetoa mchanganuo wa gharama ya Sh. bilioni 7.563 itakayotumika kukarabati kivuko cha MV. Magogoni kwa kueleza kuwa, matengenezo yake yatahusisha ununuzi wa vifaa vipya zikiwamo injini tano.

Aidha, imesema ukarabati huo ambao utafanywa na kampuni ya African Marine and General Engineering utakapokamilika utakiwezesha kivuko hicho kutoa huduma kwa miaka 14.

Taarifa iliyotolewa juzi na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ilisema ukarabati huo unatumia gharama kubwa kwa kuwa kimetumika takribani miaka 14 bila ya kufanyiwa ukarabati mkubwa.

"Sasa hivi ndiyo kinakwenda kufanyiwa ukarabati mkubwa. Katika ukarabati huo zitanunuliwa injini mpya tano ambapo nne zitafungwa kwenye kivuko na moja itakuwa ya akiba)," ilisema.

Pia ilisema fedha hizo zitanunuliwa na kufungwa marine steel plates mpya kwa sababu zilizopo hivi sasa hazifai tena kwa matumizi.

"Zitanunuliwa Gear box mpya, vifaa vya umeme na kielektroniki vipya na vifaa vingine. Vifaa vyote hivyo ambavyo ni vipya vitanunuliwa na Kampuni iliyoshinda zabuni hii ya African Marine and General Engineering Company Limited ambavyo havitengenezwi katika nchi za Tanzania na Kenya.

"Vifaa na vipuri vyote hivyo vinatoka nchi za Ujerumani, Dubai, India, Uingereza na nchi nyingine. Hivyo, kiasi kikubwa cha fedha za zabuni hiyo zitatumika kufanya manunuzi ya vifaa tajwa kutoka nchi husika," ilisisitiza taarifa hiyo.

Ilisema fedha itakayolipwa kampuni ya African Marine and General Engineering ni ndogo kuliko fedha ambayo ingelipwa kwa mzabuni wa ndani ambaye ni kampuni ya Songoro Marine Transport kama ingeshinda zabuni ingepewa Sh. bilioni 10.958.

Taarifa hiyo ilisema kampuni ya African Marine and General Engineering ni yenye uwezo wa ukarabati wa meli, boti na vivuko, boti za Azam Marine, Zanzibar 1, meli za Zanzibar zimekuwa zikikarabatiwa mara kadhaa.

Kivuko hicho kina uwezo wa kubeba tani 500 kwa maana ya abiria 2,000 na magari 60.

# Watoa mbinu kutokomeza vitabu visivyo maadili

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa elimu nchini wamesema kuzuiwa kutumika shuleni vitabu visivyo na maadili, hakutamaliza tatizo hilo iwapo mbinu zingine hazitatumika kwa kuwa vitabu hivyo vinapatikana sehemu nyingi.

Februari 13, mwaka huu, serikali ilipiga marufuku vitabu 16 kutumika shuleni kwa madai kuwa vinakinzana na mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, alisema shule itakayobainika kutumia vitabu hivyo itachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuwa uwepo wake unahatarisha malezi bora ya watoto.

Mwenyekiti wa Taifa wa Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania (TAMONGSCO), Leonard Mao, alisema juzi kuwa anaipongeza serikali kwa uamuzi iliochukua kwa kuwa utapunguza kwa kiasi fulani tatizo hilo ingawa bado kazi kubwa inahitajika kufanyika.

Alisema hiyo inatokana na kuwa vitabu hivyo husomwa zaidi nyumbani kuliko shuleni kwa kuwa watoto hununuliwa na wazazi wao kutoka kwenye maduka ya vitabu.

"Watoto wanakwenda na vitabu vya ziada shuleni na kuvisoma au huwahadithia wenzao kuwa wamesoma kitabu hiki na hiki ndipo wenzao wanakwenda kuwaambia wazazi wao wawanunulie," alisema.

Alisema serikali inapaswa kuzuia kabisa vitabu vya aina hiyo kuwapo nchini kwa kupiga marufuku kuingizwa kutoka nchi za nje, kuchapishwa au kusambazwa nchini.

"Kwa sababu kama utazuia visiwepo shuleni halafu vikaendelea kuwepo mtaani, tutakuwa hatujamaliza tatizo. Serikali ifuatilie maduka yanayouza vitabu hivyo, wawatafute wanaovichapisha na kuvisambaza hapa nchini wawafungie," alisema Leonard.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Chekechea na Msingi Ubungo, Philipine Kasoka, alisema kuna haja ya elimu kutolewa kwa wazazi juu ya vitabu bora vya ziada vya kuwanunulia watoto wao kwa kuwa wengi hawana elimu hiyo.

"Wazazi wengi hawajasoma hivyo vitabu, wanapewa tu maelekezo na watoto wao vitabu vya kununua na wenyewe wananunua na kuwakabidhi watoto bila kuvipitia na kujiridhisha na maudhui yaliyomo," alisema.

Mwalimu Maria Fwahisa aliwasihi wazazi pia kufuatilia watoto wao wanaosoma vitabu kwa njia ya mtandao kwa kuwa nako kunachangia kusambaza maudhui kinyume na utamaduni wa Mtanzania.

Alisema vitabu vingi vya ziada vinasomwa kwenye karatasi vinapatikana pia kwenye mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na wako watoto wanaovisoma kwa kutumia simu, hivyo kama na huko kusipozuiwa, tatizo litaendelea kubaki kama lilivyo.

Kiseo Joseph, mzazi wa watoto wanaosoma shule ya Kristo Mfalme, alisema serikali ikiweka wakaguzi kukagua vitabu hivyo vinapoingia nchini kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuvidhibiti visivyo na maadili kusomwa na watoto.

Alisema hiyo inatokana na wazazi kufuata maagizo ya watoto wao kwa kuwa wengi wao hawana kawaida ya kusoma vitabu hivyo, na hata walimu hawana muda wa kufuatilia mtoto anapokwenda shule na kusoma kitabu cha kiada.

"Ikiwezekana shule zifuate mtindo unaotumika kwenye shule za dini, za kuzuia watoto kwenda shuleni na vitu vyoyote vya nyumbani ikiwamo vitabu, hii inasaidia watoto kutoshawishiana kusoma vitabu hivyo, katika shule hizo watoto watumia kile kinachopatikana shule tu," alisema Joseph.


IITA Transforming African Agriculture CGIAR

INTERNACIONAL DE LA PAPA · CENTRO · CIP

## POSITION ANNOUNCEMENT
## DRIVER/FIELD ASSISTANT
## IITA-TZ2023-CIP-004-NRS-MWANZA

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Potato Center International (CIP) is seeking a Driver/Field Assistant.

Background: CIP is a not-for-profit international agricultural research organization with a global mandate to conduct research on genetic resources of potatoes, sweetpotatoes, and other Andean roots and tubers, crop genetic enhancement and improvement, integrated crop management and sustainable management of natural resources.

**Job Summary:** To drive project staff and maintain office vehicles in proper condition. This work is undertaken as part of the Sweetpotato Component of the Program for Seed System Innovations for Vegetatively Propagated Crops in Africa (PROSSIVA) implemented by the International Potato Center (CIP) and TARI. The Program for Seed System Innovation of Vegetatively propagated crops (VPCs) in Africa (PROSSIVA) will develop and validate packages of innovations to strengthen functional VPC seed systems and will work with partners to catalyze their scaling in five target countries of sub-Saharan Africa (SSA). The Sweetpotato Component aims to improve the crop's seed system through technological, marketing, and institutional innovations that deliver affordable quality seed of market-preferred varieties to actors in Tanzania in a timely manner. The Sweetpotato Component will be implemented at the Lake Zone of Tanzania. The Driver will be based in Mwanza. This position will report to PROSSIVA's Principal Investigator for the Sweetpotato Component.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Mwanza, Tanzania.

**Core Responsibilities:**
- Carrying out driving duties in a safe and courteous manner as per CIP Travel Policy and the Tanzania Traffic Act.
- Ensure use of project vehicles follows CIP motor vehicle policy, drive vehicles safely and defensively to avoid any incidents or accidents and ensure compliance with CIP driving policy in case of involvement in an accident.
- Report accidents or incidents to the supervisor in a timely manner.
- Operates, maintains, and cleans assigned vehicles with care and reports any damage immediately to the supervisor.
- Drive project vehicles for transportation of project staff to implement field activities in project target locations.
- Before proceeding on field trips ensure all travel requirements are met and liaise with staff traveling with for instructions.
- Continuously monitor the condition of assigned vehicles while driving and promptly report defects.
- Ensuring that the vehicle log sheets are filled on daily basis when the vehicle is in use. Ensure all vehicle costs incurred while in the field are reported and original receipts presented.
- Ensure that routine service and maintenance of vehicles is undertaken in a timely manner and with a reputable service provider(s)
- Assists research staff in field activities.
- Other duties that may be assigned by the supervisor.

**Qualification, Experience and Key Skills**
- Minimum of form four education.
- Minimum 5 years of professional driving experience of light and heavy vehicles.
- Must have a clean and valid Tanzania driver's license.
- Hands-on experience in simple maintenance of vehicles.
- Knowledge of defensive driving is an added advantage.
- Good knowledge of spoken and written Kiswahili. Basic knowledge of spoken and written English
- Good interpersonal skills and ability to relate well with diverse culture.
- Reliable and ability to work effectively and respectfully.

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Dar es Salaam. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

Applications: Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# Ziara za Samia, Mwinyi Oman zilivyoleta neema

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi nchini Oman imefungua neema baada ya nchi hiyo kukubali kutoa Sh. bilioni 50 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Beit-al-Jaib lililopo Forodhani visiwani Zanzibar.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi wa ziara aliyoifanya nchini Oman hivi karibuni.

Alisema ziara za viongozi hao zimefungua milango ya neema kubwa kwa jengo la Beit-al-Jaib ambalo liliporomoka zaidi ya miaka miwili linatarajiwa kujengwa upya.

Alisema Oman imekubali kutoa kiasi hicho kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo ambalo limebeba historia ya mambo ya kale ya Zanzibar katika Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Said alisema ukarabati wa jengo hilo unatarajiwa kuanza katika kipindi cha miezi mitatu ijayo ambapo kampuni iliyopewa kazi hiyo ipo katika matayarisho.

Aidha, alisema ujenzi huo utafanyika kwa kuzingatia masharti yaliopo katika mji mkongwe, ambao upo katika hifadhi ya urithi wa kimataifa wa mambo ya kale.

Waziri huyo alipongeza balozi mdogo wa Oman Zanzibar, Said Sinawi ambaye ni kiungo kikubwa katika kufikiwa kwa makubaliano ya ujenzi wa jengo la Beit-al-Jaib.

Alisema kitendo cha kuporomoka kwa jengo hilo katika kipindi cha miaka miwili limeikosesha serikali fedha nyingi zinazotokana na watalii kutembelea jengo hilo ambalo limebeba historia ya Zanzibar kupitia watawala mbalimbali.

"Ukarabati wa jengo la Beit-al-Jaib ni muhimu sana kwa upande wa Zanzibar kiasi cha kukosa mapato mengi yanayotokana na sekta ya utalii kwa wageni kutembelea jengo hilo na kujua historia ya Zanzibar,"alisema.

Hata hivyo alisema watu waliopata ajali katika jengo la Beit-al-jaib lililoporomoka watalipwa fidia kupitia kampuni ya Bima yenye makao makuu yake Tanzania Bara na serikali inaendelea kufuatilia mchakato huo.



Meneja Mawasiliano wa Hospitali ya CCBRT, Abdul Kajumulo (kushoto), akisalimiana na mmoja wa wanufaika wa huduma zitolewazo na kituo cha CCBRT Moshi kwa watu wenye ulemavu, Peter Shio, mkoani Kilimanjaro jana, wakati wa ziara ya waandishi wa habari kuelekea maadhimisho ya miaka 25 ya kituo hicho. Wengine ni wafanyakazi wa kituo hicho, Mfiziotherapia Sabas Kimario (kulia) na mtoa huduma katika jamii, Athumani Ally. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DAWASA yapewa somo uwekezaji mfumo wa kisasa

**Na Joseph Mwedapole**

MHADHIRI wa Chuo Kikuu Dar es Salaam, Dk. Richard Kimwaga, ameishauri Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuwekeza kwenye mifumo ya kisasa katika utoaji huduma za usafi wa mazingira ili kuendana na mahitaji ya ulimwengu wa sasa.

Aliyasema hayo katika mafunzo ya siku moja yaliyoandaliwa na DAWASA kwa lengo la kuongeza uelewa na usimamizi wa huduma za usafi wa mazingira ambayo yamehudhuriwa na viongozi waandamizi na watumishi wa mamlaka.

Dk. Kimwaga alisema ni wakati sahihi sasa kwa mamlaka kuangalia teknolojia kutoka kwa mataifa mengine ambao wameshaanza kutekeleza ili kuboresha sekta hii inayokua kwa kasi.

"Kuna kila sababu ya kuangalia teknolojia inayofaa katika uboreshaji wa huduma za majitaka Dar es Salaam hasa kwenye maeneo yenye wakazi wengi," alisema.

Alipongeza juhudi zinazofanywa na DAWASA katika kuhakikisha inatekeleza miradi mbalimbali ya usafi wa mazingira ili kuendana na kasi ya ukuaji wa mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Huduma za Usafi wa Mazingira wa DAWASA, Mhandisi Lydia Ndibalema, alisema mafunzo hayo ni mahususi kwa ajili ya kuongeza uelewa na ujuzi kwa watumishi ili kufahamu sekta ya usafi wa mazingira kwa undani zaidi.

"Tumeandaa mafunzo haya kwa lengo la kujikumbusha na kuongezeana ujuzi na uelewa juu ya huduma ya usafi wa mazingira kwa undani zaidi ili kuwezesha mamlaka kufikia malengo yake na kuongeza mapato kupitia mifumo ya majitaka," alisema.

Aidha, Mhandisi Hezron Magambo aliwataka watumishi wa DAWASA kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma ya usafi wa mazingira ili kuongeza uelewa juu ya manufaa yatokanayo na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya usafi wa mazingira.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) inatekeleza miradi mbalimbali ya usafi wa mazingira kwa lengo la kuboresha mazingira pamoja na kupunguza hatari ya magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

# Pesapal yahimiza matumizi teknolojia sekta ya utalii

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KAMPUNI ya huduma za malipo ya Pesapal imewataka wadau wa shughuli za utalii na ukarimu nchini kuzichangamkia na kuzitumia teknolojia za kisasa kujikwamua dhidi ya athari za janga la UVIKO-19 na kuiimarisha upya sekta hiyo muhimu.

Kwa mujibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, utalii unaingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni, unachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa na ni mwajiri wa Watanzania 600,000 ofisini na wengine zaidi ya milioni mbili waliojopatia ajira zisizo za moja kwa moja.

Maofisa Waandamizi wa Pesapal walitoa rai hiyo juzi huko Zanzibar kwenye mkutano shirikishi wa kwanza na wadau wa setka mzima ya utalii na ukarimu.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ambao waliipongeza kampuni hiyo kwa kuchagiza matumizi ya huduma za kidijitali kwenye utalii na kusisitiza umuhimu wa usalama wa mifumo ya malipo.

Katika hotuba yake, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban alisema ubunifu wa kiteknolojia na uwekezaji unaofanywa na Pesapal unaendana na ajenda ya kidijitali ya serikali.

Kiongozi huyo alibainisha kuwa wanaunga mkono kinachofanywa na kampuni hiyo kwenye shughuli za ukarimu kwani jitihada hizo zinaunga mkono mikakati na maono ya serikali ya kujenga uchumi wa kisasa ambao utategemea sana mafanikio ya sekta ya utalii.

"Teknolojia na shughuli za utalii na ukarimu ni pande mbili za sarafu moja. Wadau wa utalii wanapaswa kukumbatia teknolojia za kidijitali ili waweze kukabiliana na ubunifu unaofanyika katika sekta hii na kuweza kuyamudu mahitaji mapya ya soko, ambayo yanabadilika kwa kasi sana," Waziri Shaaban alisisitiza.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Ali Suleimani Ameir aliwataka wawekezaji wa teknolojia za kisasa kuhakikisha huduma zao zinasaidia kukuza mapato ya serikali badala ya kuwa vyanzo kwa kupotea kwake.

Ameir alisema Serikali za Muungano na Zanzibar zimeruhusu matumizi ya mifumo ya kidijitali kwa lengo la kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwamo zile za kifedha hususani malipo na miamala mingine.

Aliwataka washiriki wa mkutano huo wa Pesapal kuangalia njia na uwezekano wa kupanua huduma za malipo ya kidijitali na kuimarisha matumizi yake Zanzibar na Tanzania nzima.

Mkutano wa juzi ulijikita katika kuangalia njia ambazo teknolojia mpya zinaweza kusaidia kuimarisha uendeshaji na kuwa na vyanzo vipya na mbadala vya mapato.

Wataalamu wa Pesapal walitumia fursa hiyo kuwaonyesha na kuwahimiza wadau wa utalii umuhimu wa teknolojia katika mipango yao ya kukuza biashara na mikakati ya kuondokana na athari za UVIKO-19.

Meneja wa Pesapal Tanzania, Bupe Mwakalunda alisema kampuni hiyo ina ushirikiano wa kimkakati na mashirika ya kimataifa kusaidia kutoa suluhisho bunifu za kuimarisha huduma za utalii na ukarimu mara baada ya kupungua sana kwa janga hilo lililoikumba dunia nzima.

"Uundaji wa mifumo ya teknolojia inayoruhusu ubunifu wa haraka, kukuza faida na kuongeza ufanisi itakuwa ni kipaumbele muhimu cha kujikwamua kutoka kwenye janga ja Uviko-19 na kufikia ustahimilivu wa kidijitali," alisema na kuongeza:

"Ili kufanikisha jambo hili, tumeshirikiana na Oracle Hospitality ili kutoa suluhisho za kiteknolojia na kusaidia ushirikishwaji wa miundombinu inayoweza kunyumbulika kutoa huduma thabiti na maalumu kwa ajili ya wadau wa kisekta."

Kongamano hilo la kwanza la 'Adopt & Thrive' liliwajumuisha washiriki mbalimbali kutoka katika biashara za hoteli, migahawa, kumbi za starehe na waongoza watalii.

Pesapal na Oracle ni washirika wa karibu wa kuihudumia tasnia ya kusafiri na ukarimu nchini kupitia utaalamu na suluhisho za teknolojia mahiri ili kurahisisha na kuboresha huduma kwa watalii na wateja wengine kwa ujumla.



# Mikopo ya siri chanzo wanaume kukimbia familia Machame

**Na Godfrey Mushi,** HAI

IDADI ya wanaume wanaozikimbia ndoa zao na kutelekeza familia katika Kata ya Machame Mashariki, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, inadaiwa kuongezeka kila uchao kutokana na mikopo ya 'siri' wanayochukua mitaani.

Tatizo hilo limelisukuma Baraza la Maendeleo ya Kata hiyo, kukaa chini na kuanza kutafuta suluhu ya kudumu ya ndoa nyingi kuingia katika kufarakana, kwa sababu ya mikopo umiza inavyoziacha masikini baadhi ya familia.

Akizungumzia hali hiyo jana, Diwani wa Kata hiyo, Martin Munisi, alisema kati ya ndoa 10, ndoa sita huvunjika kutokana na baadhi ya wananchi wake kuingia katika mikopo umiza.

Alisema wengi wao walioijiingiza katika mikopo ya siri, wametumbukia kwenye lindi la umasikini hivi sasa kutokana na mikopo umiza na vicoba, kuvunja ndoa zao, huku watoto wakikosa malezi ya wazazi wawili baada ya kufarakana.

"Kutokana na kinachoendelea, tunaomba serikali kuangalia upya, asasi zinazotoa mikopo kwa kuwa zimekuwa kisababishi cha ndoa nyingi katika kata yetu na jamii kufaraka. "Kuna vikundi vinavyotoa mikopo ambavyo havipitii ofisini, wanakopesha wananchi mtaani kwa siri.Ndoa yingi zimevunjika na watoto waishi katika mazingira magumu.

"Vikundi hivi vimeleta kilio kikubwa na kusababisha wanaume kukimbia ndoa zao, wengine kujinyonga. Vikundi vinavyokopesha huku kwetu wananchi wangu wanaviita kausha damu, kwa sababu baadhi ya wakopaji wanakimbia makwao."

Kwa mujibu wa diwani huyo, haiwezekani kila sehemu kuwa na ofisi za mikopo, hivyo wanataka zichunguzwe kama zitakuwa na kibali, kwa sababu uko uwezekano wakawa hawana vibali lakini wanasumbua watu kwa kudai marejesho.

Kanuni za huduma ndogo za fedha (vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii) za mwaka 2019, kifungu cha 31, pamoja na mambo mengine zinaelekeza mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya kanuni hizo, Atakuwa ametenda kos, na atakapopatikana na hatia, atatakiwa kulipa faini isiyopungua Sh. milioni moja na isiyozidi Sh. milioni 10 au kifungo kisichopungua miezi mitatu, na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.



Meneja Mawasiliano wa Hospitali ya CCBRT, Abdul Kajumulo (kushoto), akisalimiana na mmoja wa wanufaika wa huduma zitolewazo na kituo cha CCBRT Moshi kwa watu wenye ulemavu, Peter Shio, mkoani Kilimanjaro jana, wakati wa ziara ya waandishi wa habari kuelekea maadhimisho ya miaka 25 ya kituo hicho. Wengine ni wafanyakazi wa kituo hicho, Mfiziotherapia Sabas Kimario (kulia) na mtoa huduma katika jamii, Athumani Ally. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yawapa makinikia wanawake wapate kipato

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

KAMPUNI ya uchimbaji wa madini ya tanzanite ya Franone Mining & Gem Ltd, inayofanya shughuli zake eneo la kitalu C na D, imewakumbuka wanawake wanaofanya kazi hiyo migodini, baada ya kuwapa mchanga utakaowapatia madini yatakayowasaidia kupata kipato.

Diwani wa Viti Maalum, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Paulina Makaseni, ameipongeza kampuni hiyo kwa kuona umuhimu wa kuwainua kiuchumi wanawake hao.

Alisema wamiliki wa migodi, wachimbaji na wadau wa madini ya tanzanite wanapaswa kuiga mfano wa kampuni hiyo kwa namna ilivyowakumbuka na kuwajali wanawake.

"Tunawashukuru viongozi wa Kampuni ya Franone hususani Mkurugenzi wake, Onesmo Mbise kwa kuwapa mchanga wanawake wachekechaji ili wajitafutie riziki zao," alisema

Hata hivyo alitoa wito kwa wanawake wachekechaji kupendana na kuwa na umoja katika shughuli zao ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi sambamba na kuepuka migogoro na migongano.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Kata ya Endiamtu, Claudia Dengesi, alisema hatua iliyofanywa na kampuni hiyo kwa wanawake inapaswa kupongezwa.

"Wanawake sasa hivi ndiyo wanalea familia zao hivyo tumpongeze Mkurugenzi wa Franone, Onesmo Mbise kwa kuwasaidia kina mama hao wachekechaji,"

Mwenyekiti wa UWT, Kata ya Mirerani, Johari Mwaselela, aliwashauri wamiliki wa migodi ya tanzanite, kuweka utaratibu wa kutoa mchanga wenye mabaki ya madini kwa makundi mbalimbali kwenye Jamii ya eneo hilo.

Aidha, Mwaselela alisema wamiliki hao wakiwapa wanawake udongo uliotoka kwenye buti hawatakuwa wanafanya jambo sahihi hivyo waige mfano wa Kampuni ya Franone.

# Chanzo kupungua kwa theluji Mlima Kilimanjaro chatajwa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

KUPUNGUA kwa theluji katika kilele cha Uhuru na kuchomoza kwa matukio ya uharibifu wa ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), kunatajwa kuchangiwa zaidi na ongezeko la shughuli za binadamu katika vijiji vinavyoizunguka hifadhi hiyo.

Jana Kamishna Msaidizi wa Hifadhi hiyo, Angela Nyaki, alisema sababu hizo pia zimekuwa zikisababisha upepo mkali kuvuma kuelekea kwenye mlima huo.


Kamisha Nyaki aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu maandalizi kuelekea maadhimisho ya kwanza ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa hifadhi hiyo ambayo yatafanyika Machi 16 mwaka huu. "Upepo unapotoka katika mikoa ya ukanda wa Pwani, unapokuja katika Mlima Kilimanjaro, unakuja ukiwa mkavu pamoja na joto. "Hali hiyo nayo imekuwa ikisababisha barafu kuendelea kuungua, kwa hiyo sio jukumu la Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, kuhakikisha kwamba tunapambana na mabadiliko ya tabianchini, bali pia ni jukumu la Tanzania nzima."

Kuelekea maadhimisho hayo, Kamishna huyo, alisema shughuli mbali ikiwamo usafi katika eneo la hifadhi hiyo zitaanza Machi mosi na kufikia ukomo Machi 16 mwaka huu, ambapo wadau wa utalii zaidi ya 500 wanatarajiwa kushiriki.

Alisema shughuli nyingine zitakazofanyika ni pamoja na ugawaji na upandaji wa miti, kampeni itakayozinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu.

Tangu kuanzishwa kwa shughuli za utalii katika hifadhi hiyo, mafanikio kadhaa yamepatikana ikiwamo ongezeko la watalii na kufikia 50,000 kwa mwaka, kuongezeka kwa malango ya kupanda mlima huo, kutoka mmoja hadi sita. Aidha, Naibu Kamishna wa Uhifadhi na Maendeleo ya Biashara, Herman Batiho, akizungumzia maadhimisho hayo alisema:"Maadhimisho haya ya kwanza ya aina yake yanasimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). Kimsingi, yanalenga zaidi kuutambulisha umma na dunia kwa ujumla, kwamba Mlima Kilimanjaro upo na unapatikana katika nchi ya Tanzania pekee".

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.





## Madiwani waagiza viazi vitamu kuanza kulipiwa kodi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wametaka viazi vitamu kuingizwa kwenye mfumo wa ulipaji wa kodi kama yalivyo mazao mengine ya biashara, ili kuongeza mapato ya ndani.

Wamesema zao hilo likianza kulipiwa ushuru litaongeza mapato ya halmashauri na hivyo kufikia lengo la makusanyo ya Sh. bilioni 32.6 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mazao mengine yanayotakiwa kuingizwa katika mfumo huo ni mtama, ulezi pamoja na uwele ambayo kwa sasa hayatozwi ushuru wa mazao katika masoko, minada na magulio.

Diwani wa Kata ya Sabasabini, Emmanuel Makashi aliyabainisha hayo jana katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema bila kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuvisimamia vile vya zamani itakuwa ngumu kufikia lengo la makusanyo waliojiwekea katika mwaka huu.

Alisema ili kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri ni vyema mazao ya viazi vitamu, mtama, ulezi na uwele vikaingizwa kwenye mfumo wa utozaji wa ushuru wa mazao.

Diwani mwingine, MichaelBundala alisema baadhi ya mashine za ukusanyaji wa mapato katika masoko, minada na magulio mbalimbali hazifanyi kazi na taarifa za ubovu wake zimesharipotiwa katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gagi Lala aliagiza viazi na mazao mengine ambayo hayapo kwenye mfumo wa mapato yaingizwe na ukusanyaji ufanyike mara moja.

Pia alimwagiza Mkurugenzi kuhakikisha mashine mbovu zinazotumika katika ukusanyaji wa mapato zinatengamaa ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema, halmashauri hiyo inategemea mapato yake ya ndani kwa kiwango kikubwa kupitia kilimo na wamewahamasisha wananchi kulima kwa wingi mazao ya chakula na biashara.

Alisema msimu huu pamba imelimwa kwa wingi ikilinganisha na vipindi vilivyopita na amehakikisha maofisa ugani wa kata 20 wanapata vyombo vya usafiri.

Aliongeza kuwa pikipiki 37 zimeshafika kwa ajili yao, lengo likiwa ni kuendelea kuhamasisha kilimo kwa tija ili halmashauri inapata mapato yake.

Wakati huo huo, wakulima tumbaku katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameliangukia baraza la madiwani kuliomba kuzibana kampuni zilizonunua zao hilo kuwalipa fedha.

# Serikali kuongeza idadi ya miradi inayogusa wananchi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imeahidi kuongeza miradi ya wananchi ikiwamo ya elimu ili kuwanufaisha katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi mkoani Mwanza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Ihayabuyagu na Igekemaja.

Alisema Wilaya ya Magu itaendelea kunufaika na miradi mbalimbali ya kuwaletea maendeleo wananchi kwa kuongezewa mingine 10 katika mwaka huu wa fedha.

Aliongeza kuwa hatua hiyo italenga sekta ya elimu kwenye ujenzi wa madarasa manne na maabara moja katika Shule ya Sekondari Igekemaja ambayo bado haijaanza kutumika rasmi.

Akizungumza na wananchi katika vijiji hivyo baada ya kuvitembelea na kukagua miradi inayosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), alisema serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuharakisha maendeleo ya wananchi na kwamba viongozi katika maeneo husika wanatakiwa kuisimamia.

Alisema ushirikiano wa wananchi katika kuchangia asilimia 10 ya ujenzi wa miradi inayotekelezwa na TASAF ni muhimu na kwamba umefanikisha kukamilisha nyumba ya wahudumu wa afya pamoja na vyumba vya madarasa katika shule mpya ya sekondari inayotarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni.

Mhagama alisema kutokana na uhitaji wa shule hiyo aliahidi kutatua mahitaji ya muhimu yaliyopo kwa kushirikiana na wizara zenye dhamana ikiwamo kuweka nishati ya umeme shuleni hapo pamoja na huduma ya maji.

Alisema serikali kupitia awamu ya tatu ya mradi wa TASAF itajenga maabara ya kisasa shuleni hapo pamoja na madarasa mengine manne ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa kata hiyo.

Alisema licha ya serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya TASAF kwa wakati katika maeneo mbalimbali nchini bado anashangazwa kushindwa kutekelezwa kwa muda uliopangwa, hivyo kuitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuichunguza ili kubaini kama kuna ubadhirifu.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu wa Mkoa wa Mwanza, Joachim Otaru alisema anatambua miradi hiyo ya TASAF kwa kuwa inaleta mageuzi chanya kwa wananchi wa mkoani humo.

Aliahidi kushirikiana TAKUKURU katika kuifuatilia ili kuhakikisha inaendelea kuwa na tija kwa wanufaika.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Rachel Kassanda alisema TASAF wametoa Sh. milioni 103 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya na Sh.milion 64 kujenga vyumba vya madarasa mawili ya Sekondari ya Igekemaja.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akizungumza na wananchi wa mtaa wa Igekemaja kati, kata ya Kisesa, mkoani Mwanza juzi, baada ya kukagua ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya mwalimu katika shule mpya ya sekondari inayotarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni na kumaliza mrundikano wa wanafunzi kwenye sekondari ya Kitumba yenye wanafunzi zaidi ya 2700. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wahimizwa kupata chanjo ya ugonjwa wa corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wamehimizwa kuendelea kujitokeza kupata chanjo ya ugonjwa wa corona ili kupata kinga dhidi ya ugonjwa huo endapo watapata maambukizi.

Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma mkoani Shinyanga, Mwita Thomas alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari na kuwaomba watumie kalamu zao kuhamasisha wananchi waendelee kujitokeza kupata chanjo hiyo.

Alisema ugonjwa wa corona bado upo na kwamba wananchi wanapaswa kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga ili wasipate maambukizi, ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka, kupata vitakasa mikono.

"Waandishi wa habari tumieni kalamu zenu kuongeza uelewa kwa jamii dhidi ya kupata chanjo ya ugonjwa wa corona, chanjo hii ni salama haina madhara yoyote na watu wote ambao wamechanja hakuna aliyelalamika kupata tatizo lolote na imekuwa msaada mkubwa kwao kuwakinga," alisema Mwita. Aidha, alisema katika mkoa huo wamejiwekea malengo ya kupandisha kiwango cha kuchanja wananchi hadi asilimia 120, kwamba mpaka sasa wamefikisha asilimia 108 na kubainisha kuwa chanjo hiyo inatolewa bure kwenye maeneo yote ya huduma za afya.

Ofisa Ufuatiliaji kutoka Shirika la Afya, Plus Chimombo, alisema kwa mwaka huu wanatekeleza programu ya kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya ugonjwa wa corona katika Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Kishapu na kuahidi kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari kufanya kazi pamoja.




Baada ya vitambulisho sasa kwenye stika!




**Mbunge Jafo alipotinga vijijini kukagua kero sugu za miundombinu Kisarawe**


# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 24, 2023

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe


## ZAMA ZA AWAMU YA SITA...

# Ubunifu wa 'Royal Tour' ulivyoanza kwa hadhi sumaku inayonasa 'dhahabu watalii'

- Kuzinduliwa tu, wakala kimataifa wakatua...
- Yaibua bidhaa hewa ukaa iliyoko dukani sasa

**Na Mwandishi Wetu**

ILIPOKUWA wazo hadi hatua ya utekelezaji wa Sinema ya Royal Tour, ilipata mengi ya upinzani kisiasa na huenda kijamii na kiuchumi, kwamba ni gharama kwa nchi isiyo na tija.

Ni hata mbunifu na mshiriki mkuu, Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, akaitolea maelezo machache, kwamba gharama si ya kubebeshwa serikali moja kwa moja, yenye ujumbe "ikianza mtaona thamani yake." Ni kweli sasa hali ikatoa majibu.

Hapo Rais Dk. Samia akashiriki kwenye uzinduzi wa filamu ya Tanzania The Royal Tour, katika ukumbi wa Guggenheim Museum, New York nchini Marekani Aprili mwaka jana, katika ukumbi wa Guggenheim Museum.

Hapo akapata wasaa wa kuhojiwa, naye akatumia vyema fursa hiyo kuelezea uzuri wa Tanzania kufanya utalii akiwahakikishia 'mtu hatajutia.'

Jambo mojawapo lililowavutia wengi, ni pale Rais Dk. Samia alipobainisha la ukweli na mzaha, ameendesha gari kwenye uandaaji wa filamu hiyo baada ya miaka 15 kutofanya hivyo.

Akiwa na mwongozaji maarufu wa filamu, Peter Greenberg, Rais Samia alitembelea nchini na kuonyesha wageni vivutio mbalimbali vya utalii, uwekezaji, sanaa na utamaduni vilivyopo nchini na kuwaelezea ukarimu wa Watanzania.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akishiriki kuigiza sinema ya The Royal Tour, yenye mafanikio makubwa katika sekta utalii. **PICHA: MTANDAO.**

Pia, akawafafanulia wageni nyakati za kuzuru nchini, akiutaja mwezi Juni hadi Agosti, kipindi kisicho na mvua wala joto na kwa wanaotamani kuona makundi ya wanyama yakiwa yanahama, ingawa watalii wanaweza kuja muda wowote watakao.

Lingine, ni pale akaeleza jitihada ambazo zinafanywa kuwahamasisha waigizaji wa kike na kiume kutumia vipaji vyao na sanaa kuitangaza Tanzania.

Wakati huo akasema ameshafanya mazungumzo na nchi tano zinazoongoza kwa watalii wengi Tanzania, wakikubaliana kuchukua hatua za kuisaidia sekta utalii.

Muandaaji wa filamu, Peter Greenberg, akawaahidi uzinduzi huo wa filamu ungeendelea katika maeneo mengine ya Marekani, Rais Dk. Samia akihudhuria tukio la jijini Los Angeles.

**SOKO LACHANGAMKA**

Hadi kufika mwanzoni mwa Mei mwaka jana, wiki chache tu baada ya uzinduzi Marekani, matunda ya The Royal Tour yakaanza kujionyesha nchini, wadau mbalimbali duniani wakijitokeza kuja kutathimini misitu nchini kwa ajili ya biashara ya hewa ukaa.

Rais Dk. Samia akasema katika uzinduzi wa filamu hiyo nchini jijini Dar es Salaam Mei mwaka jana, kwamba tayari ameshafanya mazungumzo na wadau wakubwa wa utalii walioonyesha ishara nzuri.

"Nimefanya mikutano kadhaa na 'giant' (vigogo) wa sekta ya utalii, nao pia baada ya kuona hii filamu, wameahidi kuja" anasema na kuendelea:

"Filamu hii imeonyesha hali ya mazingira ya Tanzania, msitu na tayari tushapokea maombi ya watu wa hewa ukaa kuja kufanya tathmini ya msitu wote waliouona, msitu wa Tanzania, ili tuanze kuvuna fedha za hewa ukaa."

Hadi sasa biashara ya ukaa imeshaanza kufanyika, ikiwamo mkoani Katavi ambayo ni kwa maslahi ya wakazi, ikiwa ni matunda ya moja kwa moja ya The Royal Tour.

**NAFASI YA TFS**

Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Tanzania, Prof. Dos Santos Silayo, mwaka jana, akasema filamu ya The Royal Tour imewasaidia kuvutia wawekezaji wengi nchini kuwekeza hususan katika biashara ya hewa ukaa.

Anaongeza kuwa wadau hao wameamua kushirikiana na Tanzania kuimarisha misitu, ili iweze kuwa sehemu ya chujio la hewa chafu duniani na kupunguza mrundikano wa gesi joto inayosababisha kuongezeka kwa joto duniani.

"Eneo la biashara ya hewa ukaa limeonekana kuwavutia wawekezaji wakubwa duniani katika bara la Asia na Marekani kuja kuwekeza na tayari kuna wawekezaji waliojitokeza tuko kwenye mazungumzo nao," anasema mkuu huyo wa TFS.

Aidha, Prof. Silayo anasema TFS imejipanga katika maeneo matatu: Kuhakikisha uhifadhi wa misitu unakuwa imara; pili kutumia maeneo ya vivutio vya misitu kuvutia wawekezaji kwenye suala la

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

TAASISI TORITA YAJA NA JIPYA...

# Wakulima tumbaku sasa kwa ubora zaidi kukausha kwa makaa ya mawe

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa TABORA**



Wakulima wakiandaa tumbaku yao **Picha : MTANDAO**

TAASISI ya Utafiti wa Tumbaku Tanzania (TORITA) imebaini njia mbadala ya kukausha Tumbaku kwa kutumia makaa ya mawe badala ya kuni, ili

kusaidia kuepusha uchafuzi wa mazingira kutokana na kukata kuni.

Ni hatua inayokuja baada ya kuonekana kuna uchafuzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini, hivyo taasisi hiyo ikaamua kubuni njia mbadala, kuwasaidia kuinuka kiuchumi wakulima wa zao hilo mkoani Tabora na kwingineko ambako zinazalishwa.

Wakulima wengi wa tumbaku, hukausha zao hilo kwa

kutumia kuni, jambo linalodaiwa kuharibu mazingira katika eneo husika.

TORITA inasema hilo ndilo limeisukuma, kuamua kufanya tafiti na kubaini njia mbadala ya kukausha tumbaku badala ya kutumia kuni na vichanja.

Hata hivyo, katika utafiti wao umebaini makaa ya mawe hukausha vizuri na kutoa tumbaku bora, inayoweza kuuzwa kokote duniani.

TORITA inasema, njia hiyo mbadala ndio suluhu kwa wakulima wa zao hilo katika maeneo mbalimbali hapa nchini, hasa ikizingatiwa zao hilo ni zao la

biashara ambalo huchangia pato la taifa.

**MKURUGENZI TORITA**

Mkurugenzi wa TORITA, Dk Jacob Lisuma, anaiambia Nipashe kuwa njia mbadala waliyoipata kukausha tumbaku kwa makaa ya mawe, pamoja na

vitofali na pumba, inatoa tumbaku bora zaidi katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi huyo anasema, njia hiyo wameipata baada ya kuona kuna uchafuzi wa mazingira pamoja na uharibifu.

"Tumebuni njia mbadala ya kuepusha kuharibu mazingira ili kusaidia serikali kupambana na uharibifu wa mazingira," anatamka mkurugenzi huyo, akifafanua kwamba ni kutokana na utafiti uliofanywa wa ukaushaji tumbaku bora, tofauti na vile jamii inavyofikiria katika maeneo mbalimbali.

Anafafanua zaidi kuwa kwa sasa tumbaku ni zao la pili kwa biashara na linachangia asilimia 17 ya Pato la Taifa, hivyo ni vyema likasimamiwa kwa weledi ili litoe mazao mengi na bora.

Kaimu Mkuu wa Rasilimaliwatu wa taasisi hiyo, Proscovia Ruzigila, anasema changamoto zinazo wakabili sasa ni pamoja na kupungua wafanyakazi, pia hawana hatimiliki za mashamba yao.

Anataja hatua walizochukua ni kufanya vikao mbalimbali na watu wa TARI na kilimo, ili kupata eneo lakini jitihada hizo bado hazijazaa matunda .

"Ukiacha maeneo ya ofisi na mashamba ,hatuna hata nyumba za wafanyakazi wala eneo la kujenga nyumba hizi, hizi ni changamoto kubwa kwetu," anasema, hatua yao wanaendelea kujipanga, ili kuhakikisha wanapata maeneo ya kudumu ya makazi yao na watumishi.

**MTAFITI**

Mtafiti wa asasi hiyo, Donatha Dunda, anasema wametumia muda mrefu kugundua njia hiyo na hivi sasa

wanafanya jitihada za kuhakikisha wakulima wanatumia njia hiyo, kwa ajili ya kukausha Tumbaku mara baada ya mavuno.

Dunda anaitaja njia hiyo ni bora sana na inaepusha uharibifu, pia kupotea kwa tumbaku, tofauti na njia nyingine ambazo hutumika na wakulima.

Anafafanua kwamba njia ya awali imekuwa ikichafua sana mazingira, hivyo matumizui ya makaa ya mawe itakuwa bora zaidi kukausha mazao yao mara baada ya kuvunwa.

Mtafiti huyo anasema, wameshapata njia hiyo wanaamini itakuwa bora na sahihi kwa wakulima wa zao la tumbaku kukaushia zao hilo.

Anaeleza imani yake kitaalamu kwamba, itawasaidia sana wakulima wengi waliokuwa wanatumia kuni kukausha tumbaku waliyovuna shambani, tayari kwa ajili ya kwenda kuiuza.

Sasa anawataka wakulima hao kuhakikisha wanazingatia njia ya kutumia makaa ya mawe, ambayo itakuwa sahihi kutokana na kwamba imefanyiwa utafiti na taasisi ya utafiti wa zao hilo nchini.

Hata hivyo, anawataka wakulima kuzingatia maelekezo wanayopewa na wataalamu wa zao hilo, ili waweze kuvuna mazao mengi na kuongeza kuwa

kilimo kinahitaji kulima kitaalam kwa kufuata maagizo ya wataalamu wa kilimo.

Mtafiti anawaelekeza wakulima kuacha kufanya kilimo cha mazoea, badala yake walime kwa kutumia utaalam na maofisa kilimo wanaowatembelea katika maeneo yao wanayolima tumbaku.

Anafafanua kuwa, tumbaku ni moja ya zao la biashara nchini na nje, hivyo ni vema wakulima wakatumia fursa hiyo kuhakikisha wanalima kitaalam kupata mazao mengi ambayo watayauza nje na nchini, kupata mapato makubwa na kuinua uchumi wao na taifa.

"Wakulima fuateni maelekezo ya maofisa kilimo,mkifanya hivyo mtafika mbali katika ukulima wa zao la kilimo,"anahitimisha Donatha.

**WALIMA TUMBAKU**

Julius Mlilo, anasema njia hiyo itawasaidia, kwanza kupunguza uchafuzi wa mazingira lakini pia itawasaidia kuepuka kupoteza tumbaku nyingi, katika kipindi cha kuikausha wakati wa kuvuna.

Anasema, kwa kutumia makaa ya mawe na vitofali vya kuchoma, itakuwa rahisi kwao kutokana na kwamba tumbaku nyingi imekuwa ikipotea kipindi cha kukausha mara baada ya mavuno.

Anasema kuwa wakulima wengi walikuwa wakitumia kuni, lakini hivi sasa makaa ya mawe yataanza kutumika ili kuhakikisha tumbaku inakaushwa vizuri.

"Tunaishukuru sana TORITA kutokana na kazi kubwa waliyoifanya ya kutupa njia mbadala ya kukausha tumbaku, maana kukaushia kuni ilikuwa Changamoto," anasema.

Mlilo anaahidi wataendelea kujifunza kutumia njia hiyo ya kukausha tumbaku mara baada itakapovunwa kutoka katika vitalu inavyolimwa.

Anasema, lengo lao ni kuona kila mkulima ananufaika na njia ya kukausha tumbaku pindi anapomaliza kuvuna na kuipeleka kwa ajili ya kuikausha tayari kwa kuingia sokoni ili ikauzwe.

# Mbunge Jafo alipotinga vijijini kukagua kero sugu za miundombinu Kisarawe

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

KATA ya Kiluvya katika wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani, ni sehemu ya mjini yenye watu wengi na inahitaji kuboreshwa miundombinu yake, lakini haijapata huduma hiyo kwa muda mrefu.

Ni hali inayoifanya ikabiliwe na kikwazo cha barabara zikiwamo mitaa, jambo linalo wakwamisha wakazi wake katika kipindi cha mvua.

Mbunge wa Kisarawe, Dk.Selemani Jafo, anasema katika kata hiyo kuna maeneo yaliyokuwa tishio kwa wananchi kuvuka kipindi cha mvua, kutokana na kukosa madaraja imara.

Hivi karibuni, mbunge Dk. Jafo alifanya ziara katika kata hiyo kukagua miundombinu na vyumba vya madarasa katika shule za sekondari Makurunge na Mloganzila.

Katika Barabara ya Makurunge, Dk Jafo alizindua daraja la Mto Makurunge, lililojengwa kuimarisha mawasiliano kati ya vijiji vya Kiluvya na Makurunge.

Ni daraja lenye urefu wa mita 10.35 lililojengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara, kwa gharama ya Sh.Mil 195.5.

Dk. Jafo ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais; Muungano na Mazingira, anasema aliiomba Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA), kujenga daraja hilo kulinda usalama wa watumiaji walioshindwa kuwasiliana wakati wa mvua.

"Niliangalia pia kwa upande wa wanawake wajawazito na watoto ambao kipindi cha mvua, kwao ilikuwa shida zaidi kupita, shughuli za wengine pia zilikuwa zinasimama" anasema.

Pia, mbunge Dk.Jafo akafika katika daraja la Mto Bululu linalounganisha vijiji vya Kiluvya na Kwakomba ni daraja hilo, lenye urefu mita 8.85 limekamilishwa kwa miezi10, kwa gharama ya Sh. milioni 123.8 fedha za Maendeleo ya Tozo la Mafuta.

Ni ujenzi ulioambatana na ukarabati wa barabara umbali wa kilomita mbili, pia mifereji vyote vinaelezwa kugharimu Sh. milioni 84.2.

Akiwa katika Kituo cha Afya Kata ya Kiluvya, akatumia nafasi hiyo kumuagiza Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kisarawe, Peter Ngusa, ahakikishe anatafuta na kupeleka fedha za kumalizia jengo la wagonjwa wa nje (OPD), pia atafute fedha za kukamilisha jengo la maabara.

Ni hatua inayotajwa, kuikomboa jamii kuacha kwenda kutibiwa katika kituo cha Afya Makurunge, umbali wa kilomita tano.

Pia, mbunge huyo akamuelekeza Meneja wa TARURA Wilayani Kisarawe, Mhandisi Godfrey Mbena, kuhakikisha anatafuta namna ya kupata fedha za kujenga kipande cha mita 500 kufika penye kituo hicho cha afya.

Safari ya mbunge huyo ikafika Shule ya Sekondari Mloganzila, ambayo imeanzishwa mwaka huu kuwaondolea kero wanafunzi waliotembea umbali mrefu kufuata shule, Sekondari Makurunge, wakitoka vijiji vya Mloganzila na Kisopwa.

"Hapa ile fedha ambayo mazazi alikuwa anaiitenga kwa ajili ya kumpa nauli mtoto, sasa atafanyia jambo lingine. Lakini, hawa wanafunzi nao watapata muda wa kurejea mapema nyumbani na kujisomea na katika hili mabadiliko ya ufaulu yataonekana" anasema.

**JAMII & UONGOZI WAO**

Ofisa Mtendaji Kata ya Kiluvya, Jonathan Juma, anasema kuna wanafuzi wasiopungua watano kila mwaka wamekuwa wakikatisha masomo, kutokana na kushindwa kumudu umbali huo, huku baadhi ya wazazi wakikwama kulipa Sh.3000 ya usafiri kwenda shule na kurudi nyumbani kila siku.

Anasema kazi iliyobaki sasa, ni kuhamasisha wanafunzi kujiunga na shule, pia kushirikiana na wazazi kutatua vikwazo ambavyo vinachangia kushuka kwa ufaulu kwenye shule za msingi na sekondari.

Mwanahawa Said, mkazi wa kata ya Kiluvya, anaishukuru serikali kuwajengea shule na kituo cha afya, vitu vilivyokuwa kikwazo kwao wananchi, hata wakalazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya.

Ally Mohamed, anayeishi Mloganzila, anasema kuwapo shule hiyo kume wapunguzia gharama wazazi na walezi, baadhi yao hata imechangia utoro kwa wanafunzi wao, kutokana na kushindwa kumudu gharama za nauli kila siku.

Mzazi mwingime ajitambulishaye kwa jina Mohamed, anaishukuru serikali kuwaondolea vikwazo vinavyokwamisha kufanya mambo mengine kwa ufanisi, kutokana na kukosa baadhi ya huduma za kijamii jirani.



Waziri Jafo akiwa ziarani Kisarawe **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Baada ya vitambulisho sasa kwenye stika!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com.

SERIKALI imekuja kivingine hakika kwa kutangaza kuondoa ukomo wa muda wa matumizi ya vitambulisho vya Taifa (NIDA) ambavyo zamani vilikuwa na muda maalumu.

Awali vitambulisho hivyo vilikuwa vinakufa baada ya miaka 10 ya matumizi yake, lakini sasa kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Masauni Yusuf Masauni, ni tumia daima unavyotaka.

Hiyo maana yake ni kwamba utabadilisha kitambulisho chako pale tu kitakapokuwa kimeharibiwa kwa sababu moja au nyingine, na kama kitakuwa kimepotea, utapatiwa kingine.

Pamoja na hoja mbalimbali zinazotolewa na wadau zikiwamo za picha kubadilishwa kutokana na mmiliki kuzeeka na kubadilika sura na ile ya utambulisho kimataifa, kutokana n a kusalia na tarehe za muda kumalizika kwenye vitambulisho, lakini uamuzi ni mzuri.

Uamuzi ni mzuri kama alivyobainisha Masauni, kwamba utapunguza kama si kuondoa kero ya kufuatilia kubadilisha, hasa kutokana na mchakato wenyewe wa kuvipata ambao umechukua miaka kadhaa, na mpaka sasa kuna watu hawana, licha ya kuingia kwenye mchakato.

Hakika, uamuzi huu hautofautiani sana na ule mwingine maarufu alioutoa Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, wa kuondoa zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa nchini.

HivisasawanasiasahususanwaUpinzaniwanajikamuahojanzitonzitomajukwaanikufahamishawananchininikilitokeakatikamiakasabailiyopita, wenginewakiitayagiza, hukubaadhiwakijishajiishananiniwanapangakuwafanyiaWatanzaniaendapowatawaparidhaanakuwakabidhinchikuongoza.

Yotekwayote, SerikalihiiimeoneshanianadhamirayadhatiyakuliwekasawaTaifahilikatikautulivu, amaninamaridhianoyanayowafanyaWatanzaniakujisikiakuwawamojanakuachadhan ayakubaguanakiitikadi,kama ilivyokuwaimeanzakukitamizizihukonyuma.

Haishangazi, kwambakatikamiakahiyosabailiyopita, Watanzaniawalibaguanawaziwazikiitikadi, hukuwapinzaniwakionekanakamawahamiajiharamuwasiotakiwakatikanchiyaoyakuzaliwa.

RaisSamiaameyakataahayoyotenasasaanakaribishakilaMtanzaniakutoaushauri, kukosoanakuisemaSerikali,laki nikwahojazenyestahanazisizo chafuawengine, ilimradinikwamustakabalimwemawanchihii.

Wakatinikipongezahatuahiyoyaserikali, namwombaWaziriMasauniageukiekeronyinginehiiambayonayohujitokezakilamwakaya Wiki yaNendakwaUsalama, ambayomadereva au wenyemagarihutakiwakupelekamagarikufanyiwaukaguziilikuthibitishausalamawao.

Hilinijambojema, linalojaliusalamawaraianamalizao, kwambagarisalamalinauhakikawausalamakwadereva wake nalenyewe,kwanihalitasababis haajalibarabarani.

Hatahivyo, ukaguzihuuwam agarinaoumekuwakamakerotu ,kwasababu kwanza hakunamaeneomahususiyakufanyiau kaguzihuo,lakinipiahakunaas kariwaukaguziwakutoshama arufukama 'maveko (vehicle inspectors)' wakuifanyashughulihiyo.

Kutokananahilo, jambohilolimekuwalikiachwamikononimwaaskariwausalamabarabarani,wanaotembeanas tikanakuziuzakwamaderevah ataambaomagariyaohayajakaguliwanamatokeoyakekugeukakitegauchumibinafsi.

Si kweli,kwambamagari yanapofanyiaukaguzihuo, hayawezikusababisha au kupataajali,hapana, ajaliziponazitaendeleakutokeakutokananasababumbalimbaliukiwamoubovuwamagari, lakinimaderevawazembenaubovuwamiondombinu.

Penginekamatukomakininajambohilo, basikipindihichopiakingetumikakuwapimaakilimaderevawote, ilikuonakamawakotimamunahivyohawawezikusababishaajaliwanapokuwabarabarani.

Kusimamishagarinakumuuziaderevastikailiaonekanegari lake limekaguliwa, sidawayakumaliza au kukomeshaajalizabarabarani, ilanikujidanganya,nanikerokusimamishanab arabaranikwakitukamahicho, hukushughulizakimaendeleozikicheleweshwa.

Hivyo, nadhaniSerikalikupitiakwaMasauni, ielewekuwakukusanyamagarieneomojakufanyiwaukaguzinijambolisilowe zekana,zaidiyakusababish akazizauzalishajikiuchumikuchelewa. Bora ukaguziwakawaidabarabaraniukaendeleakamailivyohivisasa, lakinisikwakusimamishanabilasababu.

Kufanyahivyokutakuwakumeongezasifayanchikukabiliananausumbufu, malalamikonalawamakwawatu wak e,kamailivyokuwakwenyemik utanoyahadharanavitambulis hovya NIDA. Alamsiki!

UCHUMI

# Mkopo wa 10% Halmashauri Temeke, hatua kubwa ya mfano yashuhudiwa

**Na Pilly Kigome**

HADI sasa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, nayo inang'aa kwa kuwafikia wananchi wake wenye uhitaji, familia na kwa jamii kwa ujumla, katika jitihada za kutengeneza ajira za kutosha kwa umma, ikiwa ni jukumu la kisheria kwa halmashauri zote nchini.

Kinachofanyika Temeke ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk Samia Suluhu Hassan, kukumbusha wajibu wa vyombo hivyo kutoa mikopo kwa wananchi wake na sasa Nipashe imeshuhudia inatoa nyuso za furaha kwa wakazi wake.

Ni kwamba wengi wamesha nufaika kupitia halmashauri hiyo na tayari wameshaanza kupatiwa na wengine wanakula matunda yake, kutoka pato la manispaa hiyo, asilimia 10 ya mapato yake yote yakienda kwa kinamama, vijana na wenye ulemavu.

Kupitia ushuhuda huo wa Nipashe, vijana, walemavu na wanawake ni makundi maalum yaliyolengwa na Rais tayari wameshakuwa wanufaika wa fedha zinazotolewa na halmashauri kwa kuanzisha biashara mbalimbali kwa fedha hizo.

Ni siku chache zilizopita, Manispaa ya Temeke ilitoa mafunzo maalum ya siku tatu ya ujasiriamali, ya usimamizi wa biashara na fedha kwa makundi hayo, kwa watakaofadika na asilimia 10 tajwa ya mapato ya mwaka wa fedha 2022/2023, ili kuwajengea uwezo wa kuleta tija pindi watakapopewa fedha hizo.



Washiriki wa mafunzo ya ujasiriamali na biashara ambao watafaidika na mikopo kutoka Manispaa ya Temeke. **PICHA: PILLY KIGOME.**

Katika mafunzo hayo, washiriki wameweza kunolewa kwa kupewa mbinu mbalimbali za kibiashara watakapopewa fedha hizo waweze kufanya vizuri.

**UONGOZI SERIKALINI**

Katika ufunguzi wa halfla hiyo, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Elihuruma Mabelya, akasema jumla ya vikundi 183 kutoka manispaa hiyo vimeweza kupatiwa mafunzo hayo elekezi, yaliyo wakutanisha vikundi kutoka kata tofauti kutoka ndani ya manispaa hiyo.

Anasema, sasa wanatarajia kutumia Sh. bilioni 4.6 kukopesha vikundi hivyo, ambazo tayari ziko katika mfumo.

Mbunge wa Temeke, Dorothy Kilave, anasema manispaa hiyo sasa ni ya mfano na tayari imeshatoa wanufaika wengi na matunda ya fedha hizo yako bayana.

Anasema wanatekeleza na kufuata agizo la Rais kutoa fedha kwa makundi hayo maalum elekezi, aliyoyalenga, akisisitiza: "Lakini mnatakiwa muwe waaminifu kurudisha fedha hizi kwa wakati ili na wenzenu waliobaki waweze kupewa."

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mwanahamisi Munkunda, anawafunda washiriki hao kuachana na mambo yasiyo na tija na fedha hizo, waende kufanyia kazi kama walivyopanga na kukubaliana kwa pamoja.

**WANUFAIKA WALIVYOTABASAMU**

Wakizungumza kwa furaha wanufaika hao watarajiwa, wakaiambia Nipashe kuwa, wanaishukuru serikali kuwashika mkono kuwatoa kwenye dimbwi la umasikini kutokana na mitaji hiyo.

Clara Sanga, Katibu wa kundi la Imalilo Nutrition, anasema kuwa wameanza kuwa na nyuso za tabasamu kabla hata hawajapatiwa mkopo huo, kwani inadhihirisha kuwa utaenda kuleta tija katika kundi hilo.

Anasema kundi lao limejipanga kutengeneza lishe kwa wajawazito na wagonjwa tofauti, ikiwemo na kutoa elimu kwa matumizi ya lishe hizo.

Kundi lingine ambalo limekuwa ni mfano wa kuigwa na kuonekana ni kivutio kuliko makundi yote katika mafunzo hayo ni, Jamii Partners Group, linalolenga kuanzisha biashara, kutokana na mkopo huo kutoka Manispaa ya Temeke.

Kundi hilo lililowakilishwa na vijana wawili Thomas Richard Ngelela na Alex Shauritanga, waliiambia Nipashe kuwa wao kwa pamoja na wenzao wanne, walikubaliana kuomba kiasi cha shilingi milioni 200, ili kuanzisha mradi a kituo cha afya.

Shauritanga, anasema wao ni vijana wanaojiamini na wakapitisha mpango huo, kuuwasilisha katika manispaa hiyo, hata kufikia neema ya kupitishwa.

Anasema, kwa umoja wao wote ni madaktari, watafungua kituo hicho cha afya eneo la Keko Juu, Kata ya Mgulani, wakiamini mkopo huo utaleta tija kwao.

Pia, anasema kituo hicho cha afya, kitaweza kuzalisha ajira kwa vijana wenzao wakiwemo manesi, wahudumu, walinzi na wengineo wengi.

"Tumejipanga, tumejipanga na tumejipanga tena kuhakikisha biashara yetu itakuwa na kutuletea manufaa sisi na taifa kwa ujumla" walisema

# Ubunifu wa 'Royal Tour' ulivyoanza kwa hadhi sumaku

**INATOKA UK. 11**

misitu kuvutia wawekezaji kwenye suala la utalii; na mwisho kuhakikisha kunakuwapo uwekezaji katika viwanda vya misitu na nyuki.

**MWEKEZAJI KIMATAIFA**

Kazi ya Rais Dk. Samia mwaka jana kutangazaji utalii nchini kupitia filamu The Royal Tour, zikaaendelea kuzaa matunda kwa nchi kupokea mwekezaji mkubwa wa hoteli za kifahari nchini Marekani, Munir Walji, aliyewasili kwa mazungumzo na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, kuhusu uwekezaji hoteli za kitalii.

Akaeleza ni miradi itakayoongeza thamani katika sekta hiyo ili kwenda na kasi ya ujio wa watalii nchini. Hapo Walji anaipongeza Tanzania kuweka mazingira bora yanayohamasisha kutangazwa na kuvutia wawekezaji.

Mtayarishaji sinema wa California Marekani, John Feist, naye akafika jijini Dar es Salaam, kutoa semina ya kuboresha kazi za filamu nchini akiwa na uzoefu wa miaka 22 iliyopita na nchi tisa, ikiwamo Tanzania.

**MATUNDA YA FILAMU**

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unasema, tangu Rais Samia Samia alipozinduliwa filamu ya Royal Tour, idadi ya watalii wanaotembelea utalii Ikolojia nchini, imeongezeka kutoka 49,000 kwa mwaka hadi 150,000.

Umesema kutokana na ongezeko hilio TFS nayo imeamua kuboresha njia za kupita watalii, maeneo ya malazi na kuwepo maeneo bora ya kupumzikia.

Mkuu wa Uhamasishaji wa TFS, Anna Lauwo katika Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa mwaka jana anasema watalii hao walipotembelea Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Pugu Kazimzumbwi, Dar es Salaam.

Anaitaja kuwa zao la kuunga mkono jitihada za Rais Samia, kutangaza sekta ya utalii kupitia filamu ya The Royal Tour na kuhamasisha utalii wa ndani.

"Royal Tour imehamasisha wengi kufahamu kumbe kuna utalii, kumbe Tanzania kuna kitu cha pekee ambacho sehemu nyingine hakipo na watu wameamka kumbe kuna umuhimu wa kwenda kupumzika," anasema Lauwo.

Msitu wa Pugu ulioko wilayani Kisarawe Kanda ya Mashariki, ni kati ya misitu 23 inayosimamiwa na TFS na imependishwa hadhi.

Anafafanua yana vivutio mbalimbali, ikiwamo maporomoko ya maji, mojawapo ni ya pili kwa urefu barani Afrika, kwa urefu mita 235 inayopatikana katika Hifadhi ya Kalambo, kukiwapo utalii unaofanyika kwenye mashamba ya miti yanayosamiwa na TFS, akitoa mfano wa utalii wa kuendesha baiskel.

**MAONI WIZARANI**

Aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, Juni mwaka jana akawa na ufafanuzi katika eneo hilo:"Napenda kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Rais Samia kwa juhudi zake kubwa za kuitangaza nchi yetu kimataifa kupitia programu ya Tanzania - The Royal Tour.

"Imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na wawekezaji kutembelea nchini, ambayo wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika masoko ya utalii yakiwamo Marekani, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kutembelea Tanzania kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao.

"Vilevile wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wameonyesha nia ya kuwekeza nchini kwa kujenga hoteli nne zenye hadhi ya nyota tano katika Hifadhi za Taifa Serengeti, Ziwa Manyara na Tarangire na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

"Serikali, pia imesaini mkataba wa ushirikiano katika masuala ya utalii, biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Jiji la Dallas Marekani, mwezi Aprili, 2022, hatua ambayo itafungua fursa za usafiri wa anga kwa kuwezesha safari za moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas, Marekani na kuongeza idadi ya Wageni nchini"

Akizunguzma Juni mwaka jana, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda an Biashara, Godius Khyarara, anasema ziara za Rais Dk. Samia ughabuni, pamoja na sinema ya The Royal Tour, zimeongeza pato la nchi kutoka Dola za Marekani bilioni moja (Sh. trilioni 2.3) za awali, hadi Dola bilioni 9.2 (Sh. Trilioni 21.16).

Kahyarara anasema, pia mauzo ya bidhaa nje ya nchi katika kipindi hicho yakapaa hadi Dola bilioni 10 sawa na Sh. trilioni 23, kutoka Dola bilioni saba (Sh.trilioni 16.1)



# AfDB yakunwa ujenzi Uwanja wa Ndege Msalato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UWANJA wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato jijini Dodoma unatarajiwa kukamilika Desemba 2024, huku Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ikiinidhinishwa na hatua ya ujenzi iliyofikiwa hadi sasa.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alibainisha hayo jana baada ya kuhitimisha ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa uwanja huo akiwa ameongozana na Mkurugenzi Mtendaji wa AfDB.

"Tumekuja hapa ili kukagua uwanja huu tukiwa tumeongozana na timu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wake lengo ni kuona maendeleo ya ujenzi huu kwakuwa AfDB ndiyo waliotoa fedha kwa ajili ya ujenzi huu,"alisema.

Alieleza mradi huo wa uwanja unajumuisha awamu ya kwanza ambayo ni ujenzi wa njia ya kuruka na kutua kwa ndege ya kilomita 3.6 utakao gharimu Sh.bilioni 164.

"Awamu ya pili itakuwa ni ujenzi wa jengo la abiria ambalo litakuwa na uwezo wa kuhudumia watu milioni mbili kwa mwaka na linatarajia kugharimu kiasi cha Sh.bilioni 194.4."

"Kazi ipo vizuri sisi kama serikali tumeridhika na mgeni wetu kutoka AFDB, na yeye pia ameridhishwa na ujenzi namna unavyoendelea,"alisisitiza Prof. Mbarawa.

Aidha, alisema sehemu ya kwanza ya ujenzi inayohusisha ujenzi wa eneo la ndege kutua na kuruka mpaka imefikia asilimia 15 na kwa upande wa sehemu ya pili ya ujenzi wa majengo na miundombinu mingine bado mkandarasi yuko katika hatua ya maandalizi. Mkurugenzi Mtendaji wa AfDB, Jonathan Nzayikorera alimshukuru na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake imara na maono aliyonayo katika mradi huo.

"Nitaenda kusema nilichokiona, maendeleo ni mazuri sana, nimefurahishwa na kasi ya ujenzi inavyoenda lakini niwaombe makandarasi kuhakikisha kuwa wanatekeleza na kufanya kazi kwa wakati ili mradi huu ukamilike ndani ya muda," alisema Nzayikorera.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mhandisi Rogatus Mativila, alisema sehemu ya kwanza ya mradi huo imefikia asilimia 15 kwa kuwa mkataba wa ujenzi wake ulisainiwa mapema mwaka 2021 wakati ujenzi wa sehemu ya pili ya ujenzi wa majengo ulisainiwa mwaka 2022.

"Wakati Rais Samia akiweka jiwe la msingi kuashiria ufunguzi wa ujenzi huu aliwataka makandarasi wa ujenzi wa mradi huu kufanya kazi kwa bidii na kuhakikisha kuwa mradi unakamilika mapema iwezekanavyo." "Uwanja huu ni wa kimataifa, ukikamilika utaleta mapinduzi makubwa Dodoma kwa kuwa ndege kubwa zilizokuwa zinashindwa kutua zitatua sasa na hata wageni wakubwa wanaokuja kuonana na Rais badala ya kutua KIA au JNIA watatua Dodoma moja kwa moja," alisema Mativila.



Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Lusako Kilembe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio ya wakala huo mkoa kwa kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Utoaji siri taasisi nyeti za serikali kwamchefua Katibu Mkuu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, Kaspar Mmuya amekemea tabia ya utoaji wa siri za taasisi nyeti akisema ni ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma.

Amesema kwa mtumishi yoyote atakayebainika atachukuliwa hatua kali.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha baraza la wafanyakazi wa wizara hiyo kilichofanyika jijini jana.

Mmuya alisema mafanikio ya wizara hiyo yanatokana na siri na unyeti wa taarifa ambazo zipo nchini.

"Naomba nisisitize suala la usiri katika utendaji kazi wenu siyo tunajadili mambo yetu baada ya muda mchache unayakuta katika mtandao hiyo haikubaliki, kama hamtokuwa wavumilivu hamtatenda haki,"alisema.

Akizungumzia kuhusiana na mikutano ya siasa ya hadhara, alisema tangu mikutano hiyo ianze wananchi wanafurahi hakuna vurugu yoyote inatokea na wananchi wanalindwa.

"Hakuna changamoto katika mikutano ya hadahara, nawashukuru viongozi wa siasa kwa kuwa wanatambua nao ni jukumu lao kuleta amani ya nchi ili ujumbe wanaoutaka ufike kwa wananchi," alisema.

"Wakiwa na mikutano wanaleta ratiba zao nasi tunaangalia kama kuna changamoto tunazitatua,"alisema.

Alisema Jeshi la Polisi jukumu lao ni kulinda ili matokeo anayotaka Rais kwa wananchi wake yaende vizuri.

Kamishna wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali watu, Suzan Kaganda, alisema Jeshi la Polisi litaendelea kusimamia amani na utulivu katika nchi, huku akisisitiza limejipanga katika masuala ya usalama barabarani ili kuhakikisha ajali za barabarani zinapungua.

# Bil.6.4/- zatengwa kuimarisha uthibiti ubora vyuo vikuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 6.4 kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi(HEET) kwa ajili ya kuimarisha uthibiti ubora na uhuishaji wa mitaala ya vyuo vikuu.

Zaidi ya mitaala 300 ya vyuo vikuu iko katika hatua mbalimbali za kufanyiwa mapitio ili kuhuishwa kwa kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali ili kukidhi matarajio yao na mahitaji ya soko.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) Prof. Charles Kihampa, alibanisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za tume hiyo kwa waandishi wa habari. "Katika kufanikisha hili tume imeendelea kuandaa na kuratibu mafunzo ya kubadilishana uzoefu kwa viongozi na wanataaluma wa vyuo vikuu kuhusiana na uendeshaji wa vyuo vikuu, utengenezaji mitaala inayozingatia ujuzi na inayoendana na soko."

"Mbinu za ufundishaji kwa wahadhiri ambao hawakusoma fani za ualimu, ulinganifu wa programu za masomo, uthibiti ubora na utengenezaji na utumiaji wa mifumo ya kompyuta"alisema

Pia, alisema katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022 jumla ya viongozi na wanataaluma 575, wamenufaika na mafunzo hayo ambayo yamelipiwa na serikali kwa asilimia 100.

"Kutokana na hatua hizi zinazochukuliwa na serikali, vyuo vikuu vimeweza kuimarisha mifumo yake ya uthibiti ubora na uendeshaji wa mafunzo,"alisema.

Aidha, alisema serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo azma yake ya kuongeza wigo wa fursa za masomo ya elimu ya juu kwa Watanzania. "Nafasi za masomo katika vyuo vya elimu ya juu katika programu za shahada ya kwanza zimeongezeka kutoka 157,770 mwaka 2020/21 hadi 172,168 mwaka 2022/23,hili ni ongezeko la nafasi 14,398 sawa na asilimia 9.1,"alisema.

Kadhalika, alisema programu za masomo ambazo zimeruhusiwa kudahili wanafunzi wa shahada ya kwanza zimeongezeka kutoka 686 mwaka 2020/21 hadi 757 mwaka 2022/23. Vile vile, alisema wanaodahiliwa katika shahada ya kwanza wameongezeka kutoka 87,934 mwaka 2020/21 hadi 113,383 mwaka 2022/23 sawa na asilimia 28.9.

"Pia idadi ya wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu imeongezeka kutoka 259,266 mwaka 2020/21 hadi 295,919 mwaka 2021/22 sawa na asilimia 14.1, idadi hii inatarajiwa kuongezeka kwa mwaka wa masomo 2022/2023,"alisema





# Hospitali ya Rufani yapokea mashine ya upumuaji watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya imepokea msaada wa vitanda saba na mashine mbili za kuwasaidia watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya wakati kupumua ili kuokoa maisha yao.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa juzi kwa uongozi wa hospitali hiyo na taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Doris Mollel Foundation na kupokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Doris Mollel alisema vifaa hivyo vina thamani ya Sh. milioni 13 na kwamba aliamua kuvitoa kwa ajili ya kushirikiana na serikali kupunguza vifo vya watoto hao wanaozaliwa kabla ya wakati.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati na hivyo jitihada za kukabiliana na vifo vya watoto hao zinatakiwa ziongezeke kwa ushirikiao kati ya serikali na wadau.

"Mimi ni miongoni mwa watu waliozaliwa kabla ya wakati lakini nilihudumiwa vizuri kwa sababu mama yangu alikuwa ni muuguzi, kwahiyo niliamua kuanzisha taasisi hii ili niwasaidie watoto hawa wahudumiwe kama mimi nilivyohudumiwa," alisema Doris.

Alisema alipeleka vifaa hivyo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya baada ya kupata maombi kutoka kwa viongozi mbalimbali wa mkoa huo akiwemo Mbunge wa Mbeya Mjini na Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson.

Alisema mashine hizo za kupumulia zina uwezo wa kuwahudumia watoto wanne kwa wakati mmoja na hivyo akawaomba wahudumu wa hospitali hiyo kuvitumia vifaa hivyo vizuri ili vitumike kwa muda mrefu.

Daktari Bingwa wa Watoto katika hospitali hiyo, Dk. Alinanuswe Kasililika alisema kwa mwezi huwa wanapokea watoto wanaozaliwa kabla ya wakati kati ya 25 na 50 huku kitengo hicho kikiwa na uwezo wa vitanda 37.

Alisema wakati mwingine kunapokuwa na msongamano wa watoto hao, huwa wanalazimika kuwalaza wawili kwenye kila kitanda jambo ambalo alisema miongozo ya afya hairuhusu kutokana na kuwa na uwezekano wa kuambukizana magonjwa.

Alisema watoto wanaozaliwa kabla ya wakati huwa wanapoteza maisha endapo watakosa mashine za kuwasaidia kwenye upumuaji na hivyo kitendo cha kuongezewa mashine mbili kwenye idara hiyo kitasaidia kukabiliana na vifo hivyo.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Elesia George alimshukuru Mkurugenzi wa Taasisi hiyo ya Doris Mollel Foundation kwa msaada huo akieleza kuwa utasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa uliopo kwa sasa.

Alisema Mkoa wa Mbeya una vituo 14 vya kulelea watoto wanaozaliwa kabla ya wakati na kwamba vyote vinahitaji kuwa na vifaa kama vilivyopelekwa katika hospitali hiyo ili kupunguza msongamano kwenye hospitali hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliwataka wafanyakazi wa hospitali hiyo kuvitumia vizuri vifaa hivyo ili vitumike kwa muda mrefu kuokoa maisha ya watoto na kuwatia moyo adau wanaosaidia.

Alimuomba Mkurugenzi wa Taasisi hiyo kuendelea kusaidia vifaa hivyo kwenye vituo vingine ndani ya mkoa huo kwa maelezo kuwa bado uhitaji ni mkubwa.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akimshukuru Mkurugenzi wa Taasisi ya Doris Mollel Foundation, Doris Mollel baada ya kupokea msaada wa vifaa vya kusaidia kuokoa maisha ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti), alivyo vitoa kwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Uchakavu miundombinu wahatarisha maisha ya wanafunzi shule ya msingi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Nyeregete katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wapo hatarini kuangukiwa na kuta za madarasa kutokana na uchakavu wa miundombinu ya shule hiyo.

Aidha baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wanalazimika kukaa chini kutokana na shule hiyo kukabiliwa na upungufu wa madawati.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Amina Mwachuma aliyasema hayo wakati wa kupokea msaada wa madawati 100 kutoka kwa Jumuiya ya Nyeregete.

Alisema shule hiyo ina hali mbaya ambayo inahatarisha maisha ya wanafunzi kwa maelezo kuwa baadhi ya madarasa yanya nyufa kutokana na shule hiyo kuwa ya siku nyingi.

Aliiomba Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kusaidia kuboresha miundombinu hiyo kabla haijaleta madhara kwa wanafunzi wa shule hiyo.

"Hali ya shule yetu siyo nzuri kabisa, kuta zina nyufa na hatari kwa maisha ya watoto wetu, tunaiomba serikali iliangalie hili ili watoto wetu wasome kwenye mazingira mazuri," alisema Mwachuma.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Nyeregete, Tumain Mpande alisema shule yake ina zaidi ya wanafunzi 600 na kwamba mbali na uchakavu wa majengo pia inakabiliwa na tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo.

Vilevile alisema shule hiyo inada idadi ndogo ya walimu ambayo inawalazimu walipo kubeba mzigo mkubwa wa kufundisha masomo mengi bila kupumzika ambapo alisema shule hiyo ina walimu sita pekee.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbarali, Missana Kwangura alisema Halmashauri itahakikisha inafanya jitihada mbalimbali ili kutatua tatizo hilo kwa kutumia fedha zinazotokana na mapato ya ndani pamoja na zinazotoka serikali kuu.

Akizungumza kwa niaba ya wana jumuiya ya Kijiji cha Ngeregete, Fransica Mjengwa alisema lengo alisema kwa awamu ya kwanza walikabidhi madawati 34 lakini lengo lao ni kufikisha madawati 100.

Alisema lengo lao ni kushirikiana na serikali kutatua kero hiyo ambayo imekuwa inaweza kukwamisha sekta ya elimu katika kijiji chao.

# Watoto wafariki madai kunywa dawa za kienyeji, baba akamatwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia mkazi wa Kitongoji cha Kitete kilichopo Kata ya Bwawani katika Wilaya ya Chunya, Makeremo Luhaga, kutokana na watoto wake wawili kufariki dunia baada ya kunywa vitu vinavyodhaniwa kuwa ni dawa za kienyeji.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga alisema jeshi hilo lilimkamata mzazi huyo Februari 20 kwa ajili ya mahojiano.

Alisema jeshi hilo lilipokea taarifa za vifo vya watoto hao, Februari 19, mwaka huu kuwa watoto wa mzee huyo walifariki baada ya kunywa dawa walizopewa na mganga wa kienyeji aliyefahamika kwa jina moja la Galwinzi.

Kamanda Kuzaga alisema watoto wa mzee huyo waliofariki ni Raphael Makeremo (26) na Mafunda Makeremo (18) ambao wote ni wakazi wa kitongoji hicho cha kitete.

Alisema watu wengine watatu wa familia hiyo walilazwa hospitalini baada ya kunywa dawa hiyo na kwamba baada ya tukio hilo mganga aliyewanywesha dawa hiyo alitimka na kutokomea kusikojulikana.

Aliwataja waliolazwa hospitalini kuwa ni Nchambi Lusangija (50) ambaye ni mama wa familia, Manyilizu Kulyehewa (07) na Njile Makeremo (18) na kwamba watu hao wanaendelea vizuri.

"Uchunguzi wa awali umebaini kuwa chanzo cha tukio hili ni imani za kishirikina kutokana na watoto wa familia ya mzee Luhanga kusumbuliwa na maradhi ya tumbo na vichomi kwa muda mrefu hivyo kuamini matatizo hayo yanatokana na kulogwa," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema Jeshi hilo linaendelea na msako wa kumtafuta mganga wa kienyeji ambaye aliwanywesha dawa wanafamilia hao ili achukuliwe hatua za kisheria.

Kamanda Kuzaga aliitaka jamii kuachana na imani potofu za kishirikina kwa maelezo kuwa zinasababisha madhara makubwa kwa jamii na badala yake watafute tiba ya maradhi yanayowasumbua kwa kwenda hospitalini.

Aidha aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuwatumia waganga wa kienyeji wasio na vibali ambao wana walaghai kuwatibu kwa kutumia dawa za kienyeji kwa lengo la kujipatia kipato pasipo kuwa na uelewa wa dawa wanazozitoa bila vibali.

# Bil. 140/- zawekezwa Kisiwa cha Bawe, Changuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

DOLA za Marekani milioni 60 (Sh. bilioni 140.7) zimewekezwa katika visiwa vya Bawe na Changuu vilivyopo katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja ambazo zimetokona na ukodishwaji wa visiwa hivyo.

Uwekezaji huo umefanywa na Kampuni ya KOKUN KOLEKSHEN ambao ni wamiliki wa Kampuni ya LA ROSA DEIVENT Zanzibar na hatua hiyo ni muendelezo wa ukodishwaji wa visiwa vidogo vilivyopo ndani ya Zanzibar ambapo Serikali imeshakodisha visiwa 16.

Akizungumza jana katika hafla ya makabidhiano ya visiwa hivyo vya Bawe na Changuu iliofanyika katika Kisiwa cha Changuu , Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadha Soraga, alisema uwekezaji huo utasaidia katika sekta ya kiuchumi na kutoa fursa ya ajira kwa wananchi.

Waziri Soraga alisema uwekezaji katika visiwa ni suala mtambuka na sekta zote za serikali zinawajibu wa kushirikiana kwa pamoja ili kulinda mila, silka na utamaduni.

Hivyo, alimtaka muwekezaji wa visiwa hivyo, kuhifadhi mazingira ya visiwa kwa sababu mazingira katika kisiwa yanamambo mengi na kama hatokuwa makini itaathiri haiba ya visiwa.

Aidha, alimtaka muwekezaji huyo kuzingatia miiko ya uhifadhi wa mazingira ikiwamo ujenzi na uhifadhi wa taka ngumu, nyepesi na maji ya mabwawa ya ambayo yanakiwango kikubwa cha klorin.

Pia alimtaka muwekezaji huyo kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana wa maeneo ya karibu ya kisiwa kwa sababu mcheza kwao hutunzwa, hivyo wale wanaoshi karibu kuwa wanufaika wa mwanzo wa mradi huo.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, alimtaka muwekezaji huyo kuwa na usimamizi mzuri wa rasilimali zilizokuwamo katika kisiwa hicho ambazo ni hazina za nchi ikiwamo majengo ya urithi na viumbe hai kama vile kobe.

"Kisiwa hiki cha Changuu kinahistoria nyingi, kinamajengo ya urithi yaliojengwa miaka 200 iliyopita lakini pia kuna maliasili nyingi ikiwemo wanyama kama kobe kwa ajili ya manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo"alisema Simai.

Waziri wa Uchumi wa buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, alisema maendeleo ya uchumi wa buluu na uvuvi yanategemea visiwa kwa sababu eneo hilo limezungukwa na bahari.

Alisema katika bahari kunashughuli mbalimbali ambazo zinahusiana na uhifadhi wa bahari na bila ya uhifadhi hakuna maendeleo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Sahrif Ali Sharif, alisema mchakato wa ukodishaji wa visiwa wa kampuni hiyo imepata visiwa viwili Changuu na Baweh na visiwa hivyo vinahistoria kubwa hivyo ni muhimu vitunzwe na vilindwe.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Idrisa Kitwana alisema serikali inawekeza katika visiwa lengo ni kuwanufaisha pande zote mbili, muwekezaji na serikali ili kuhudumia jamii.

Mkurugenzi wa Kampuni ya KAKUN KOLEKSHEN, Andrea Azzola, alisema malengo yake ni kuunga mkono juhudi za serikali katika uwekezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo ya sekta ya utalii.

Alisema kampuni yake imefanya utafiti na kubaini kuwa Zanzibar ni eneo zuri la kimkakati katika uwekezaji wa miradi ya kiutalii.Alisema licha ya kuwekeza katika visiwa hivyo lakini ataimarisha uhusiano mzuri na wananchi wanaozunguka miradi hiyo kama alivyofanya katika miradi mingine huko Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Zanzibar inavisiwa vidogo 54 kati ya hivyo visiwa 16 vimeshakodishwa ambavyo ni Bawe, Changuu, Pamunda A, Pamunda B, Chapwani, Pungume, Kibandiko, Kwale, Misali, Mtangani, Kashani, Matumbini, Njao, Niamembe, Miwi na Kwata.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya uwekezaji na vitega uchumi Zanzibar (ZIPA), Sahrif Ali Sharif (kulia), akizungumza na Mwekezaji wa Kisiwa cha Changuu na Bawe, Andrea Davide Azzola (katikati), katika hafla ya makabidhiano ya visiwa hivyo, Mkoa wa Mjini Magharib, Unguja jana, baada ya serikali kumkodisha muwekezaji huyo kwa zaidi ya dola za kimarekani milioni 60. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM Zanzibar yaeleza mafanikio ya Samia miaka miwili

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Chama Mapinduzi (CCM) Zanzibar, kimesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameonyesha uwezo mkubwa katika kulitumikia taifa na kuimarisha uhusiano wa kimataifa.

Hayo yalisemwa na Katibu wa Idara ya itikadi, Uenezi na Habari, Khamis Mbeto Khamis wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi kuu za chama hicho, kuhusu miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia kushika wadhifa huo. Mbeto alisema kwamba barabara za kuunganisha mikoa zinajengwa kwa kasi pamoja na zile za wilaya na sasa serikali imeelekeza nguvu katika ujenzi wa barabara za vijijini.

Alisema mradi unaondelea wa ujenzi wa wa reli ya treni ya umeme utakapokamilika utafungua mlango wa kiuchumi ndani ya nchi pamoja na nchi jirani. Alisema kwamba fedha za ugonjwa wa corona zimesaidia miradi mingi ya maendeleo katika sekta ya afya, elimu na Zanzibar imekuwa mnufaika mkubwa. Mbeto alisema uongozi wa Rais Samia, uhusiano wa kimataifa unaendelea kuimarika pamoja na serikali kufanikiwa kuimarisha uhuru wa vyombo vya hababri ambao ulianza kuzorota katika siku za nyuma.

Akizungumzia maendeleo yaliopatikana Zanzibar katika uongozi wa Rais D.k Hussein Ali Mwinyi alisema miradi mingi ya kimaendeleo imekuwa ikichomoza katika sekta ya afya, elimu, uvuvi pamoja na kufanikiwa kuimarisha misinngi ya utawala bora.

# Wizara ya Afya yajipanga kukabiliana na maradhi tishio

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema imejipanga kukabiliana na maradhi ambayo ni tishio kwa afya ya binaadamu ikiwemo homa ya ini na UKIMWI kwa kushirikiana na Taasisi ya CDC kutoka Marekani.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya Wizara katika kupambana na maradhi ambayo ni tishio kwa afya ya binaadamu.

Mazrui alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na CDC wanakusudia kutekeleza mradi wa miaka mitano ambao utaiwezesha Zanzibar kupambana na maradhi yanayosababisha athari za afya za binaadamu.

Alisema ugonjwa wa Ukimwi bado tishio licha ya kuwapo kwa mikakati ya kupunguza kasi yake ikiwemo matumizi ya dawa za kufubaza makali.

Aidha, alisema maambukizi ya UKIMWI kwa upande wa Zanzibar yapo kwa asilimia 0.15, huku mikakati ya Wizara ni kupambana kwa kuyafikia makundi hatarishi.

# RPC mstaafu: Mtuhumiwa atoe maelezo awali kortini

**Na Restuta James**

KAMANDA na Kachero mwandamizi mstaafu wa Polisi, SACP Jamal Rwambow amependekeza marekebisho ya sheria, ili maelezo ya awali anayotoa mtuhumiwa kituo cha polisi, yasitumike kama ushahidi mahakamini.

SACP Rwambow aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipowasilisha maoni yake kwenye Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Hakijinai inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande.

Alisema mtuhumiwa anaweza kutoa maelezo ya awali polisi kwenye mazingira magumu pale anapokutana na askari wasio na uadilifu.

"Nimewaambia hiyo inaweza kuwa chanzo cha malalamiko mengi, maana baadhi ya wapelelezi wasio na uadilifu, wanatumia njia zisizo halali kupata maelezo. Nimewaambia wajaribu kuangalia ungamo (kukiri kosa) lilipatikanaje," alieleza.

Alisema wananchi wanapoibua malalamiko kuhusu jeshi hilo, hususani kubambikwa kesi, yachunguzwe na hatua zichukuliwe kwa wahusika.

Alisema sababu za malalamiko ya raia kubambikiwa kesi ni uvivu wa baadhi ya polisi na wapelelezi katika kufanya kazi zao.

"Wakati mwingine jeshi linawapa watu majukumu ya kupeleleza au kusimamia upelelezi wakati ujuzi na uwezo wao ni mdogo. Sasa wakiwapa wataalamu wanaoweza kupeleleza, wanaweza kabisa wakapunguza malalamiko hayo," alisema.

Afande Rwambow ambaye kabla ya kustaafu, alikuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni na kisha kuongoza kitengo cha teknolojia ya mawasiliano, alisema ili kuwapata wapelelezi makini, jeshi hilo linapaswa kuzingatia mwongozo wake wa utendaji kazi (PGO).

SACP Rwambow aliweka angalizo la kuwapo kasoro za kiutendaji kwa polisi wakati wa upelelezi, inapotokea jukumu anakabidhiwa asiye na weledi.

"Kwa kukiuka hayo (PGO) wanaweza wakajikuta hawawapati wapelelezi. Kwa hiyo, watu wanaingia katika shughuli za upelelezi wakati hawana ujuzi wa kupeleleza," alisema.

Pia alipendekeza waendesha mashtaka wa serikali, wawe ni wanasheria wenye ujuzi wa upelelezi ili wanapoandaa kesi kupeleka mahakamani, wawe wamejiridhisha. Alisema jambo hilo litapunguza msongamano wa mahabusu. Pia alipendekeza kuweka motisha kwa watoa taarifa kwa wapelelezi ili kurahisisha kazi hiyo, pia vifaa zaidi kwa askari wanaofanya kazi hizo.

Akizungumzia kushikiliwa kwa muda mrefu kwa mahabusu, alisema PGO inaelekeza ukaguzi wa mara kwa mara wa wakuu wa vituo na kuongea na watuhumiwa, hivyo kazi hiyo ikifanyika kwa usahihi, tatizo hilo litapungua.

"Kuna hali ya kupuuzia miongozo ya Jeshi la Polisi... malalamiko mengi yanayotolewa kwa polisi yanaweza kutatuliwa na wao wenyewe," alisema.

Alisema wapo askari wenye dhamana ya kukagua mahabusu za polisi pamoja na mafaili ya watuhumiwa kabla kesi hazijaenda mahakamani, jambo ambalo limepuuzwa na baadhi ya wenye wajibu huo.

Kuhusu nafasi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamanda Rwambow alipendekeza kuwa mamlaka inayoteua wasadizi wa kiongozi huyo, ihakikishe wawe na uwezo wa kuwawajibisha watakaoshindwa kutimiza majukumu yao ipasavyo.

Kwa muundo wa Jeshi la Polisi, hivi sasa IGP anasaidiwa na makamishna saba ambao Kamanda Rwambow anapendekeza wawe chini ya Kamishna Mwandamizi watakayewajibika kwake badala ya hivi sasa wote wanakwenda moja kwa moja kwa IGP.

Alisema jambo hilo litaongeza nidhamu kwa kuwa hivi sasa IGP hana nguvu ya kuwawajibisha makamishna wasiomsaidia.

Kuhusu ajira, Kamanda Rwambow alisema miongozo na taratibu ya polisi ikisimamiwa vizuri inaweza kuondoa ajira za 'kujuana' ndani ya jeshi na pia amependekeza sifa za kujiunga na jeshi hilo zisiwe tu kwa waliopita Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Kamishna Mkuu wa Magereza mstaafu, Augustino Nanyaro alisema amewasilisha marekebisho ya maeneo tisa ikiwamo sheria ya magereza ili taasisi hiyo ifanye kazi kwa ufanisi katika mazingira ya sasa.

Alisema sheria ya magereza pamoja na kanuni zake vinapaswa kurekebishwa kwa kuwa kwa namna ilivyo, kuna namna inaminya utendaji wa jeshi hilo katika mazingira ya sasa.

## Wajasiriamali 10,000 kunufaika na mikopo

**Na Gwamaka Alipipi**

WAJASIRIAMALI wadogo na wa kati zaidi ya 10,000 nchini wanatarajia kunufaika na mikopo itakayowawezesha kujiendeleza na kupanua biashara zao kitaifa na kimataifa.

Mbali na kupata mikopo, pia watapatiwa elimu ya masuala ya fedha, ujuzi wa kufahamu fursa na maendeleo ya biashara ulimwenguni.

Mratibu wa mtandao unaohusiana na masuala ya maendeleo na ukuaji wa kiuchumi (Accelerate Africa) Tanzania, Pendo Lema alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mtandao huo nchini.

"Lazima tuanze na vikundi vya wafanyabiashara wadogo na wale wa kati kwani wengi wao hawana uelewa wa fursa nyingi za biashara zilizoko na ambazo wakizifahamu na kuzitumia vizuri watanufaika zaidi," alisema Pendo.

Alisema hatua hiyo pia itawasaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati kuchangamkia fursa zilizoko kwa kupata uelewa wa kutosha kuhusiana na maendeleo ya biashara kwenye mataifa mbalimbali ulimwenguni.

Alisema mtandao huo nchini una mpango wa kuanzisha programu itakayoitwa 'operesheni ya mafunzo kwa wajasiriamali 100,000 kwa nchi 10 za Afrika' ambayo itawawezesha wajasiriamali kupata ufadhili wa fedha.

Mratibu wa Accelerate Afrika Kanda ya Afrika, Gilbert Ewehmeh alisema: "Mfumo wetu huu unalenga kuunda biashara endelevu kwa nia ya kuimarisha sekta ya viwanda ili kuondoa umasikini na kuhakikisha uwapo wa uchumi endelevu".

Alisema mtandao huo umejikita zaidi kwenye nchi za Afrika kutokana na kuwapo na matatizo yanayohusiana na masuala ya kiuchumi.

Ewehmeh alisema ni wakati mwafaka kwa wanachama kutumia fursa zitokanazo na eneo huru la biashara la Afrika ambazo hazina ufahamu kuhusiana na fursa hizo.

Alizitaja nchi ambazo ni wanachama wa mtandao huo ni Botwana, Cameroon, Malawi, Ghana, Rwanda, Afrika Kusini, Uganda, Kenya, Tanzania na Zimbabwe.



Mratibu wa mtandao wa Accelerate Africa, Pendo Lema (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mkutano wa kwanza wa wafanyabiashara wadogo wanaoanza kuwekeza na wale wa vikundi vya wafanyabiashara wadogo na wa kati jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi rasmi wa mtandao huo hapa nchini. Kulia ni Mratibu wa Mtandao huo Barani Africa, Gilbert Ewehmeh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wawakilishi wa vyuo vikuu bora duniani watua nchini

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO vikuu bora vya nchi za India, Cyprus, Malaysia na Uturuki vimetuma wawakilishi wake nchini kuonyesha shughuli zao kwa Watanzania wanaotaka kusoma kwenye nchi hizo.

Vyuo hivyo vitafanya maonyesho kwenye Hoteli ya Serena kesho na kwamba keshokutwa watafanya maonyesho kama hayo kwenye viwanya vya Mapinduzi Square Zanzibar.

Mkurugenzi wa Global Education Link (GEL), Abdulmalick Mollel ambaye ndiye mwenyeji wa vyuo hivyo, alibainisha hayo jana jijini alipozungumzia ujio wa vyuo hivyo.

Aliwataka vijana Watanzania kuchangamkia fursa hiyo kwa kuhudhuria maonyesho ya vyuo hivyo ili wachague kozi wanazotaka kwenda kusoma nje ya nchi.

Alisema baadhi ya vyuo vikuu vilivyokuja vinafundisha uhandisi wa meli, urubani na baadhi vina viwanda vya kutengenezea magari.

"Kuna vyuo vimepunguza ada za masomo ya udaktari wa tiba kutoka Sh. milioni 30 kwa mwaka hadi Sh. milioni 10 kwa mwaka. Hii tunaona ni fursa sana kwa Watanzania kuchangamkia na watakaofika, watapata udahili siku hiyo hiyo bure," alisema Mollel.

Alivitaja vyuo vya India ambavyo vimeleta wawakilishi wake ni pamoja na Lovely Professional (LPU) ambacho kimebobea kwenye elimu ya uhandisi na biashara, Chuo Kikuu cha MMU ambacho kimebobea kwenye elimu ya tiba na uhandisi na Chuo Kikuu cha Sharda ambacho kimebobea kwenye elimu ya tiba, sanaa na biashara.

Alitaja vyuo vingine kuwa ni vya Cyprus kama Near East University kilichoko Kaskazini mwa nchi hiyo, Chuo Kikuu cha Kyrenia wakati nchi ya Uturuki vyuo vilivyotuma wawakilishi ni Gelism na Ishiki na Malasyia ni Chuo Kikuu cha Segi.

Alisema vyuo vikuu vya Uingereza navyo vimetuma wawakilishi kupitia taasisi ya British Council.

Alisema India ina vyuo vikuu vingi, hivyo vyuo vikuu ambavyo GEL imeviomba vije ni vyuo vikuu bora nchini humo na kwamba vimeletwa kimkakati.

Alisema vyuo hivyo vinatoa kozi ambazo nyingi hazitolewi kwenye vyuo vya ndani na hata kama zinatolewa, nafasi ni chache.

"Tumeleta vyuo vikuu vilivyobobea kwenye uhandisi wa aina zote - mafuta, gesi madaraja, reli kwa sababu tunaona ujenzi wa reli ya kisasa (SGR). Kwa hiyo, tunatambua uhitaji wa wataalamu wa aina hii hapa Tanzania siku zijazo," alisema Mollel.

Alisema wameleta pia vyuo ambavyo vitawafundisha vijana kusimamia mifumo ya kwenye mafuta na gesi pamoja na bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda kwenda Tanga.

# CHAMA, ZIMBWE JR, AZIZ KI RASMI MABALOZI CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imesaini mkataba wa makubaliano na wachezaji, Clatous Chama, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' , Aziz Ki na Farid Mussa kutoka Simba na Yanga kuwa mabalozi wa kufikisha elimu ya fedha kwa jamii kupitia kampeni yake ya "Benki ni SimBanking."

Mikataba na wachezaji hao imesainiwa katika makao makuu ya CRDB na kushuhudiwa na viongozi waandamizi kutoka benki hiyo pamoja na viongozi wa Simba na Yanga.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema CRDB kwa muda mrefu imekuwa ikishiriki katika kusaidia jitihada mbalimbali za kimichezo kwa kutambua mbali ya michezo ni burudani, bali pia michezo ni biashara na uchumi pia.

**Nsekela alisema katika kipindi cha miaka mi tatu iliyopita CRDB im eanzisha mbio za ki mataifa za hisani za CRDB Bank Marathon, mashindano ya taifa ya mpira wa kikapu na mashindano ya resi za Ngalawa.**

"Pamoja na juhudi zetu za kuwekeza katika michezo mingine lakini Benki ya CRDB pia imewekeza katika mchezo wa mpira wa miguu kupitia ufadhili ambao tumekua tukitoa kwa klabu ya Namungo, lakini pia mwaka jana tulishirikiana na vilabu hivi vya Simba na Yanga katika maandalizi ya Simba Day pamoja na Wiki ya Mwananchi kama maandalizi ya msimu mpya wa ligi kuu ya soka ya Tanzania bara" aliongeza Nsekela.

Benki ya CRDB imefikia hatua ya kusaini makubaliano na wachezaji hao wa Simba na Yanga ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuongeza wigo wa ufahamu wa elimu ya fedha kwa wachezaji wa soka na jamii kwa ujumla lakini pia ikiwa pia ni sehemu ya kutambua viwango vizuri ambavyo vimeonyeshwa na wachezaji hao katika kusaidia timu zao kupata matokeo mazuri lakini pia nidhamu ambayo wameonyesha katika mchezo jambo ambalo ni muhimu sana kwa mafanikio ya mchezaji.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine, ameishukuru CRDB kwa kutoa ubalozi kwa wachezaji wao jambo ambalo litaleta hamasa kwa wachezaji wengine kuongeza juhudi jambo ambalo litaisadia klabu wakati huu inaposhiriki mashindao ya ndani na nje ya nchi.

"Tunaishukuru CRDB kwa kuwatambua wachezaji wetu na kuwapa heshima hii kubwa ya kuwa mabalozi wao. Kwa kuwa mabalozi wa taasisi kubwa kama Benki ya CRDB kunaleta imani na hamasa hata kwa taasisi nyingine kutaka kushirikiana na wachezaji wetu jambo ambalo litanuifaisha sio tu wachezaji bali vilabu na soka letu kwa ujumla wake" alsema Mtine.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, naye amepongeza hatua ya Benki ya CRDB kuwatambua wachezaji wao na hasa kwa kuangalia mchango wao katika timu na nidhamu jambo ambalo ni muhimu kwa mafanikio yao na timu kwa ujumla.




Timu ya Wafanyakazi wa Betika ambayo inashiriki mashindano ya soka maalumu ili kuhamasisha utunzaji wa mazingira. Kikosi hicho kilifungwa mabao 3-1 na Coco Beach katika mechi ya ufunguzi iliyochezwa Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Nane kuchuana Sodo Climate*

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU nane zitachuana kusaka bingwa wa mashindano maalumu ya kuhamasisha utunzaji wa mazingira yaliyoandaliwa na Kampuni ya Michezo ya kubashiri ya Betika Tanzania.

Ligi hiyo iliyopewa jina la Betika Sodo 4 Climate, mbali na uwanjani, pia inahamasisha washiriki na jamii kuhusu utunzaji wa mazingira kupitia mchezo wa sodo.

Meneja Mkuu wa Betika Tanzania, Tumaini Maligana, alisema ligi hiyo ina kauli mbiu ya Shabikia Soka sio uharibifu wa mazingira.

"Lengo ni kushiriki katika kutokomeza uharibifu wa mazingira unaosababisha athari za mabadiliko ya tabia za nchi.

Tunapotunza mazingira tunakuwa na hali ya hewa nzuri, afya bora na pia maendeleo katika jamii yetu," alisema Maligana.

Alizitaja timu zitakazochuana ni Wafanyakazi wa Betika, Coco Beach, RC FC, Tulia Trust Foundation, Espanyol, Bodaboda Msasani na IPP Media.

Ligi hiyo ilizinduliwa rasmi juzi na katika mechi ya ufunguzi Coco Beach waliwachapa Betika Staff mabao 3-1.

## Kidunda aingia mitini, kushtakiwa

**Na Saada Akida**

BONDIA, Selemani Kidunda, hatapanda ulingoni kupigana na Patrick Mukala kutoka Jamhuri ya Kidemkorasia ya Congo (DRC), kutokana na kutoonekana katika zoezi la kupima uzito.

Katibu wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), Yahya Poli, alisema Kidunda hatashiriki pambano hilo kwa sababu amekiuka kanuni za mchezo huo.

"Kwa mujibu wa sheria na mchezo wa ngumi, bondia analazimika kupima uzito siku moja kabla ya pambano, tumeshuhudia wote Patrick Mukala amepima na Kidunda hajatokea, kwa mantiki hiyo pambano halitakuwepo," alisema Poli.

Promota wa pambano hilo, Saadah Salum, alisema mabondia wanapaswa kuwa na nidhamu na kuacha kusikiliza maneno ya watu baada ya kusaini mkataba wa kucheza pambano husika.

"Sina taarifa yoyote ya bondia Kidunda kama atatokea kucheza, nitafuata taratibu za kisheria, kwa sababu amesaini mkataba kila kitu kipo wazi," Saada aliongeza.

Mapambano mengine yaliyopangwa kufanyika leo kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam, yataendelea kama kawaida.

## Klabu 13 kuchuana kuogelea Taliss-IST

**Na Saada Akida**

KLABU 13 zimethibitisha kushiriki katika mashindano ya kuogelea ya Taliss-IST yaliyopangwa kufanyika Jumamosi na Jumapili kwenye bwawa la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) Masaki, Dar es Salaam.

Meneja wa Klabu ya Taliss-IST, Hadija Shebe, amezitaja klabu hizo ni Dar es Salaam Swim Club (DSC), Bluefin, Morogoro Piranhas, Mwanza Swim Club, Wahoo Zanzibar, FK Blue Marlins, Uganda Flash Swim, Braeburn (Arusha), Premiere Swim (Dar es Salaam), Mwanza Swim Club, Lake Swim Club, Taliss-IST na HPT.

Alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na waogeleaji wanafanya mazoezi ili kupambana na kuzinyakua zawadi mbalimbali zitakazotolewa siku hiyo.

Aliongeza waogeleaji zaidi ya 200 wanatarajia kushiriki katika mashindano hayo yaliyodhaminiwa na IST, Bwana Sukari, Pepsi, Jubilee Insurance, Dehli Darbaar, Wrap and Roll, F and L Juices na Burgers 53.

Alieleza waogeleaji watashindana katika umri na staili mbalimbali kwa mujibu wa taratibu.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FRESNEDA AGEUKA LULU

KLABU ya Arsenal iko tayari kumenyana na Borussia Dortmund, Newcastle na Juventus katika kuwania huduma ya beki wa kulia wa Real Valladolid, raia wa Hispania, Ivan Fresneda, 18. (***Standard***)

### PICKFORD MAMBO SAFI

KIPA wa Timu ya Taifa ya England, Jordan Pickford, mwenye umri wa miaka 28 anakaribia kusaini mkataba mpya na Everton. (***Times***)

### ARSENAL, XHAKA KITAELEWEKA

ARSENAL imeanza mazungumzo ya kuongeza mkataba na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uswisi, Granit Xhaka, mwenye umri wa miaka 30, ambaye ana nia ya kusalia Emirates. ( ***90,min***)

### GVARDIOL ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanavutiwa na mlinzi wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri miaka 21. ***(Fabrizio Romano)***

### CANCELO ATOBOA SIRI

MLINZI wa Ureno, Joao Cancelo (28), amesema uhamisho wake wa mkopo kwenda Bayern Munich ilikuwa fursa ambayo hangeweza kuikataa baada ya kuamini anafaa kucheza zaidi Manchester City, huku Kocha, Pep Guardiola, akipinga. (***O Jogo, via Mail)***

### MUDRYK SOKONI TENA

MKURUGENZI wa Shakhtar Donetsk, Darijo Srna, amesema klabu hiyo itajaribu kumsajili tena fowadi wa Ukraine mwenye umri wa miaka 22, Mykhailo Mudryk, siku zijazo baada ya kuhamia Chelsea mwezi uliopita. (***Football Ramble, via Football.london)***

### SABITZER KUBAKIA UNITED

WAKALA wa kiungo wa kati wa Austria, Marcel Sabitzer, amedokeza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anaweza kusalia Manchester United hadi mwisho wa msimu huu kutokana na uhamisho wake wa mkopo kutoka Bayern Munich. (***Sport 1***)

### NAPOLI KUMUUZA OSIMHEN

RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis, ameipa Manchester United matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa Nigeria Victor Osimhen (24), baada ya kusema "wakati mwingine kuna ofa ambazo huwezi kuzikataa". (***Mirror***)

### DAHOUD ANUKIA LEICESTER

KLABU ya Leicester City inaweza kuanza mchakato wa kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na Ujerumani, Mahmoud Dahoud, mwenye umri wa miaka 27 kwa mkataba wa uhamisho wa bila malipo msimu wa joto. (***Leicester Mercury***)

### FOSTER: SIJUTII CHOCHOTE

KIPA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Ben Foster, mwenye umri wa miaka 39, amesema hajutii kukataa nafasi ya kustaafu na kusaini Newcastle. (***TalkSPORT***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: SIKUTARAJIA CITY KUIFUNGA BAYERN

### ●●● Ni kutokana na changamoto ya ratiba na ubora wa vigogo wa Bundesliga...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola alifurahishwa na alichokiona licha ya baadhi ya watu kutarajia ushindi wa moja kwa moja kwa Manchester City dhidi ya RB Leipzig.

Guardiola hakufurahi mapendekezo Manchester City walitarajia kuishinda kwa raha RB Leipzig baada ya kutoka sare ya bao1-1 kwenye mechi yao ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Riyad Mahrez aliifungia City bao la kuongoza dakika ya 27 katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Red Bull Arena juzi usiku, huku City wakiwa na nguvu kubwa katika kipindi cha kwanza cha mkondo wa kwanza nchini Ujerumani.

Lakini vijana wa Guardiola hawakutumia vyema udhibiti wao na Leipzig ikasawazisha kupitia, Josko Gvardiol na mechi yao ya marudiano itakayochezwa Machi 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Etihad.

Kikosi cha Marco Rose kiko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga na kilikuwa hakijafunga bao katika mechi tatu zilizopita za mtoano za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, Guardiola alikataa madai kwamba walipaswa kushinda dhidi ya Leipzig.

Aliiambia BT Sport: "Watu walitarajia tutashinda magoli 5-0, hiyo sio ukweli. "Imepita hatua ya makundi katika mashindano yenye ushindani mkubwa na timu nyingi muhimu.

"Ni vigumu, tulijua hili, mchezo wetu wa nne ndani ya siku 10, michezo ya ugenini, safari na watu wanatarajia ushindi kitu ambacho sio sawa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,080,3

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEYMAR SASA KUIKOSA BAYERN



**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR amepata majeraha ya kifundo cha mguu na huenda akashindwa kuivaa Bayern Munich itakapoikabili Paris Saint-Germain katika mechi ya pili ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alitolewa nje kwa machela wakati PSG iliposhinda mabao 4-3 dhidi ya Lille Jumapili iliyopita.

Baada ya kufunga bao la pili la PSG, Neymar aliumia kifundo cha mguu wake wa kulia katika changamoto na Benjamin Andre mapema kipindi cha pili.

PSG ilithibitisha baadaye Neymar hajaumia lakini sasa imethibitika kuwa aliumia.

Kwa mujibu wa gazeti ma France Football, muda wa kawaida wa kupona jeraha kama hilo ni kati ya wiki sita na nane, hali itakayomfanya akose mechi ya pili itakayochezwa Machi 8, mwaka huu.

PSG, ambao watamenyana na Marseille kwenye Ligue 1 keshokuwa wataelekea Munich wakiwa nyuma kwa bao 1-0.



# Henry: Kiwango cha Lukaku kimepanda

**MILAN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Romelu Lukaku, anaonekana katika hali nzuri zaidi kuliko hapo awali, kwa mujibu wa kocha msaidizi wake wa zamani wa Ubelgiji, Thierry Henry.

Lukaku aliingia akitokea benchi dakika ya 58 dhidi ya Porto juzi kabla ya kupachika bao pekee katika ushindi wa mkondo wa kwanza wa hatua ya 16 bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Inter Milan, Beppe Marotta, alikuwa ametilia shaka utimamu wa Lukaku alipoiambia Sky Sport fowadi huyo "anahitaji kuwa na umbo kamilifu ili aweze kuwa fiti. Lakini Lukaku, anayecheza kwa mkopo Inter akitokea Chelsea, alitoa majibu kamili alipofunga bao pekee dakika ya 86.

"Nina furaha sana kwa Rom," alisema Henry akiiambia CBS Sports. "Anaonekana fiti zaidi. "Nadhani alikatishwa tamaa hakuanza, jibu pekee unaweza kutoka ni uwanjani, na alifanya hivyo.

Mustakabali wa Lukaku bado haujulikani kwani hadi sasa haujaeleweka wakati wa msimu wake wa mkopo wa muda mrefu akiwa na Inter, akifunga mara nne katika mechi 14.

Hata hivyo, kurejea kwake Chelsea muhula uliopita kulikatisha tamaa vile vile.

"Tulikuwa na mazungumzo alipokwenda Chelsea, na nikamwambia atapata ugumu kucheza Chelsea."

## HABARI MICHEZO

318,061/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Aston Villa | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 02. 25/02/23 | 18:00 | Birmingham City vs Luton Town | 2.90 | 3.15 | 2.45 |
| 03. 25/02/23 | 18:00 | Bristol City vs Hull City | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 04. 25/02/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Blackburn Rovers | 2.45 | 3.25 | 2.85 |
| 05. 25/02/23 | 18:00 | Stoke City vs Millwall FC | 2.49 | 3.15 | 2.85 |
| 06. 25/02/23 | 18:00 | West Bromwich Albion vs Middlesbrough FC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 07. 25/02/23 | 18:15 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.85 | 3.10 | 2.55 |
| 08. 25/02/23 | 20:30 | Schalke 04 vs VfB Stuttgart | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 09. 25/02/23 | 21:00 | Maritimo Madeira vs Santa Clara Azores | 2.50 | 3.10 | 2.85 |
| 10. 25/02/23 | 22:45 | US Lecce vs Sassuolo Calcio | 2.41 | 3.20 | 2.95 |
| 11. 25/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.85 | 3.20 | 2.48 |
| 12. 26/02/23 | 16:30 | Tottenham Hotspur vs Chelsea FC | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 13. 26/02/23 | 17:00 | FC Nantes vs Stade Rennes | 3.20 | 3.20 | 2.23 |
| 14. 26/02/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs Strasbourg Alsace | 2.28 | 3.20 | 3.15 |
| 15. 26/02/23 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.37 | 3.40 | 2.85 |
| 16. 26/02/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs GD Chaves | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 26/02/23 | 18:30 | FC Lugano vs FC Basel 1893 | 2.45 | 3.25 | 2.36 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 24/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4677 | Mohammedan SC vs Sreenidi Deccan FC | 2.23 | 3.42 | 2.79 |
| 15:00 | 1430 | Kukesi vs Partizani Tirana | 3.21 | 2.85 | 2.29 |
| 15:00 | 3123 | Bylis Ballsh vs Egnatia Rrogozhine | 3.04 | 2.79 | 2.42 |
| 16:00 | 3084 | Ruvu Shooting vs Kagera Sugar | 2.48 | 2.63 | 3.16 |
| 16:00 | 3481 | Johor Darul Takzim vs Terengganu | 1.29 | 4.50 | 7.00 |
| 16:00 | 3485 | Shabab Al Dhahiriya vs Hilal Al-Quds | 3.84 | 3.22 | 1.89 |
| 16:00 | 4141 | Hadiya Hosahina FC vs Ethiopian Medhin | 2.80 | 2.80 | 2.59 |
| 16:00 | 5566 | Etincelles vs AS Kigali | 3.21 | 2.90 | 2.26 |
| 16:50 | 2451 | AL Khalidiyah vs Manama Club | 2.69 | 3.00 | 2.53 |
| 16:50 | 3051 | Al Hidd Club vs East Riffa | 2.60 | 3.02 | 2.60 |
| 18:00 | 1021 | Sabayil vs Gabala | 3.99 | 3.26 | 1.84 |
| 18:00 | 2171 | Vojvodina vs Radnik Surduluca | 1.43 | 4.11 | 6.45 |
| 18:00 | 3771 | KF Erzeni vs Laci | 2.41 | 2.80 | 2.70 |
| 19:00 | 2951 | HNK Sibenik vs Istra | 2.86 | 2.96 | 2.42 |
| 19:00 | 3158 | U Craiova SA vs CS Mioveni | 1.67 | 3.22 | 5.91 |
| 19:00 | 3761 | Legetafo Legedadi vs Mekelakeya | 5.61 | 3.69 | 1.54 |
| 19:00 | 4456 | Dodoma FC vs Ihefu FC | 2.47 | 2.85 | 3.20 |
| 19:30 | 1622 | Sport Podbrezova vs Zemplin Michalovce | 1.78 | 3.47 | 3.99 |
| 20:00 | 1180 | Pafos FC vs Aris Limassol | 2.05 | 3.26 | 3.63 |
| 20:00 | 1612 | Cukaricki St vs Kolubara | 1.34 | 4.36 | 8.09 |
| 20:00 | 3136 | Doxa Katokopia vs Karmiotissa | 2.15 | 3.36 | 3.25 |
| 20:30 | 3629 | SuperSport Utd vs Maritzburg Utd | 1.87 | 3.23 | 4.23 |
| 21:00 | 1840 | CD Trofense vs Penafiel | 3.21 | 3.10 | 2.22 |
| 21:00 | 3769 | Nordsjalland vs Odense | 1.73 | 3.88 | 4.18 |
| 21:00 | 3782 | Volos vs Lamia | 1.61 | 3.76 | 5.30 |
| 21:30 | 1106 | Bastia Borgo vs Nancy | 3.77 | 3.35 | 1.92 |
| 21:30 | 1199 | Chateauroux vs Orleans | 2.08 | 3.21 | 3.42 |
| 21:30 | 4225 | Red Star vs Avranches | 1.47 | 3.99 | 6.51 |
| 21:30 | 4556 | UTA Arad vs Farul Constanta | 3.12 | 3.12 | 2.28 |
| 22:00 | 2322 | Roda Kerkrade vs Almere City | 2.33 | 3.36 | 2.79 |
| 22:00 | 2782 | Heracles Almelo vs Telstar | 1.56 | 3.99 | 5.14 |
| 22:00 | 2984 | VVV Venlo vs FC Oss | 1.58 | 4.00 | 4.95 |
| 22:00 | 3019 | Willem II Tilburg vs Jong Ajax | 1.41 | 4.71 | 6.07 |
| 22:00 | 4214 | NAC Breda vs Dordrecht | 1.70 | 3.84 | 4.21 |
| 22:00 | 4928 | Helmond Sport vs Jong Utrecht | 2.24 | 3.42 | 2.89 |
| 22:00 | 5557 | Sparta Rotterdam vs Utrecht | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 22:00 | 5971 | FC Eindhoven vs De Graafschap | 2.49 | 3.21 | 2.68 |
| 22:30 | 2808 | Mainz vs Monchengladbach | 2.02 | 3.58 | 3.28 |
| 22:30 | 5531 | Frosinone vs Parma | 2.08 | 3.17 | 3.53 |
| 22:30 | 5886 | LASK Linz vs Austria Lustenau | 1.42 | 4.46 | 5.81 |
| 22:45 | 1696 | UCD Dublin vs Sligo Rovers | 3.78 | 3.37 | 1.86 |
| 22:45 | 2484 | Bohemians FC vs Dundalk FC | 2.65 | 3.12 | 2.49 |
| 22:45 | 5097 | Derry City vs Cork City | 1.35 | 4.35 | 7.87 |
| 22:45 | 5621 | St Patricks vs Shelbourne | 1.99 | 3.22 | 3.48 |
| 22:45 | 5767 | Raith Rovers vs Ayr United | 2.46 | 3.26 | 2.68 |
| 23:00 | 2483 | Eibar vs Villarreal B | 1.71 | 3.41 | 4.94 |
| 23:00 | 3710 | Fulham vs Wolverhampton | 2.27 | 3.23 | 3.03 |
| 23:00 | 4642 | Elche vs Betis | 3.74 | 3.39 | 1.97 |
| 23:00 | 5383 | Lille vs Brest | 1.34 | 4.98 | 7.97 |
| 23:15 | 2432 | Famalicao vs Portimonense | 1.90 | 3.34 | 3.99 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MCHENGERWA MGENI RASMI KILIMANJARO MARATHON 2023

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mbio za Kimataifa za Kilimanjaro za mwaka huu zitakazofanyika keshokutwa Moshi, mkoani Kilimanjaro, imefahamika.

Mchengerwa amethibitisha kushiriki hafla hiyo na ataongozana na viongozi wengine wa ngazi ya Mkoa wa Kilimanjaro na wa ngazi ya Kitaifa katika shughuli hiyo.

"Wakati wa hafla hiyo, Waziri Mchengerwa anatarajiwa kuanzisha rasmi mbio za kilomita 42 na zile za kilomita 21, halafu yeye mwenyewe kushiriki mbio za kilomita tano za Granda Malt", ilisema sehemu ya taarifa ya waandaaji wa mbio hizo.

Taarifa hiyo iliendelea kusema maandalizi yote yamekamilika na maonyesho maalum yajakulikanayo kama Kili Expo yanayotangulia tukio la mbio yalianza tangu jana kwenye viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU).

Taarifa hiyo imeeleza kuwa katika maonyesho hayo wadhamini mbalimbali wa mbio hizo za kimataifa wanatarajiwa kuonyesha bidhaa, huduma na shughuli mbalimbali wanazozifanya kupitia taasisi zao.

Taarifa hiyo pia imeeleza maonyesho hayo ya siku nne yanaenda sambamba na ukusanyaji wa namba na vifaa kwa ajili ya washiriki wa mbio hizo katika viwanja vya MoCU huku wito ukitolewa kwa washiriki kuzingatia muda na siku zilizowekwa kwa ajili ya uchukuaji namba.

"Kamati ya wandaaji pia inatoa onyo kwa wale wanaoendesha zoezi haramu za kuuza tiketi za bandia kwenye mitandao, hawa wanafuatiliwa kwa makini na watakapobainika, hatua kazi za kisheria zitachukuliwa dhidi yao", ilisema taarifa hiyo.




Mkazi wa Musoma, mkoani Mara, Mwaliki Nyangasi, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 6.7 baada ya kushinda Jackpot bonus ya SportPesa kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya mechi 13 za Jackpot zilizochezwa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Nabi awacharukia 'wazembe' Yanga*

INATOKA UK 24

hiyo inawaweka kwenye mazingira magumu kuelekea mwisho wa msimu.

"Ni kweli hatuko katika nafasi nzuri kwenye msimamo, tunaenda kufanyia kazi mapungufu yetu ili kujiandaa na michezo ijayo, shida ya timu hatuwezi kuweka mambo ya kifamilia mbele za watu na kupambana kumaliza ndani kwa ndani," Hitimana alisema.

Yanga ndio mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inashirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

## Simba yawatisha Vipers FC, Mkude...

INATOKA UK 24

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha timu hiyo kipo imara na wameenda Uganda kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya tu.

Ahmed alisema mechi hiyo itakuwa ndio fainali yao kutokana na kushikilia mustakabali hatima ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Tumejipanga, matumaini yetu yote Wanasimba yapo kwenye mechi hii dhidi ya Vipers. Mustakabali wa ushiriki wetu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu huu utaamuliwa na dakika 90 za pale Entebbe. Sisi kama Simba tumejidhatiti, tutaondoka na alama tatu pale Uganda ili kujiweka sawa kwenye vita yetu ya kuitafuta nusu fainali msimu huu," alisema Ahmed.

Aliongeza kwa kuwapa salamu kutoka kwa Rais wa heshima wa Simba, Mohamed Dewji na Bodi yake ya Wakurugenzi ya kutokata tamaa na kuendelea kushikamana katika wakati huu mgumu na waamini yatakaa sawa.

"Tumeona hata timu mbalimbali barani Ulaya, mfano Liverpool ni mbabe sana, linapokuja suala la mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini mmeona kilichomkuta dhidi ya Real Madrid. Ni kawaida kwa timu ambayo inayojitafuta na kujitengeneza upya baada ya kutamba kwa muda," Ahmed alisema.

Simba inaburuza mkia katika Kundi D baada ya kufungwa bao 1-0 na Horoya AC ya Guinea na ilikubali kichapo cha magoli 3-0 kutoka kwa Raja Casablanca ilipowavaa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# Michezo

Nipashe

Ijumaa Februari 24, 2023


UKURASA 22



## Henry: Kiwango cha Lukaku kimepanda




Winga wa Yanga, Dickson Ambundo (kulia), akipambana kumiliki mpira dhidi ya mchezaji wa KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda bao **1-0. PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba yawatisha Vipers FC, Mkude...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkongwe, Jonas Mkude, Jimmyson Mwanuke, Augustine Okrah na chipukizi Mohammed Mussa, wameachwa katika kikosi cha Simba kilichoondoka nchini jana kuelekea Uganda kwa ajili ya kuwakabili wenyeji, Vipers FC kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho jijini, Kampala.

Msafara wa Simba umeondoka ukiwa na wachezaji 25 na lengo moja la kusaka ushindi ili kurejesha matumaini ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kusafiri, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' alisema tayari amelinasa faili ya Vipers na kujipanga vyema namna watakavyoikabili.

Robertinho alisema anafahamu vyema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kwa sababu kila upande unahitaji pointi tatu ili kufufua 'mwanga' kuendelea na michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

"Ninaifahamu vizuri Vipers, tumewaandaa wachezaji kimbinu, kiufundi na kisaikolojia ili kufikia malengo ya kusaka ushindi katika mchezo huo," alisema Robertinho.

Kocha huyo aliongeza anatumia ubora na madhaifu ya wapinzani wao kwa ajili ya kutafuta matokeo yanayotarajiwa na mashabiki na wanachama wa Simba yatakayowarejeshea furaha ambayo wanaisubiri.

INAENDELEA UK 23

# *Nabi awacharukia 'wazembe' Yanga*

## ●●● Awataka nyota wasiojituma kubadilika huku akitabiria makubwa CAF...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuondoka na pointi tatu muhimu, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amewatolea uvivu baadhi ya wachezaji wake kwa kucheza kiwango cha chini katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

**Wachezaji walioanza katika mechi hiyo iliyomalizika kwa vinara hao kupata ushindi wa bao 1-0 ni pamoja na Djigui Di arra, Shomari Kibwana, David Bryson, Ibrahim Bacca, Bakari Mwamnyeto, Zawadi Mauya Tuisila Kisinda, Salum Abuba kari 'Sureboy', Clement Mzize, Stephane Aziz Ki na Dickson Ambundo.**

Hata hivyo, baada ya mechi hiyo, kikosi cha Yanga kiliondoka nchini na kuanza safari ya kuelekea Mali kuwafuata Real Bamako kwa ajili ya mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa keshokutwa.

Nabi aliliambia gazeti hili hakutarajia kuona kikosi alichokipanga kikionyesha kiwango kibovu tofauti na matarajio yake.

Kocha huyo alisema alitumia mchezo huo kuwapumzisha baadhi ya nyota waliocheza mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe na kuwapa nafasi wenzao ambao hawakupata namba katika mchezo uliopita.

Alisema alitarajia kutokana na nguvu waliyokuwa nayo, alitarajia wangeonyesha kiwango bora na kumshawishi kuelekea michezo mingine inayofuata.

"Wachezaji wamesajiliwa ili kucheza, hata wale ambao walikuwa hawachezi, wanapopata nafasi ya kuvaa jezi ya Yanga lazima waonyeshe kitu walichonacho, unapewa nafasi unashindwa kuonyesha, kuna wengine tangu nijiunge na Yanga miaka miwili iliyopita kiwango chao ni kile kile.

Hawabadiliki, hawaonyeshi tofauti na wakiwekwa nje mara fulani hachezi mara mwingine anacheza, ndio maana mechi ya leo (juzi), wachezaji waliopewa nafasi hawakutaka kujituma kwa kuonyesha kile walichonacho," alisema Nabi.

Aliongeza hajafurahishwa na kitendo cha wachezaji waliopata nafasi kutojituma na kutoonyesha kiwango kizuri cha kupambania timu licha ya kutengeneza nafasi nyingi za wazi.

Alieleza alilazimika kufanya mabadiliko ya kikosi kwa kuwapa mapumziko nyota wake ili kuwandaa vyema na mchezo ujao wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Real Bamako ya Mali.

"Sikuwatumia wachezaji wote ambao walicheza mechi ya TP Mazembe kwa sababu wachezaji hao watatumika katika mechi yetu ya Kombe la Shirikisho dhidi ya timu ya Mali (Real Bamako)," alisema Nabi.

Kocha Mkuu wa KMC , Thierry Hitimana alisema mechi dhidi ya Yanga ilikuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu walikutana na timu kongwe iliyotoka kupata matokeo mazuri katika michuano ya kimataifa dhidi ya TP Mazembe.

Hitimana alisema wamecheza wakiwa na presha ya kutafuta matokeo chanya ya haraka huku Yanga nayo ikihitaji alama tatu muhimu ili kuendelea kujiimarisha kileleni.

"Tumecheza na timu kubwa, mipango yetu ni kucheza kwa kuzuia, Yanga wasipate bao lakini tumefanya makosa kwa kipa na kuwapa ushindi Yanga," alisema Hitimana.

Aliongeza anasikitika kuona timu yake inaendelea kuvuna matokeo mabaya katika michezo ya hivi karibuni na hali

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >